# Nipashe

Jumatano Aprili 20, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580921

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US



SportPesa

TZS. 1,171,243,460


BET LEO UWE BILIONEA

SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#




**Polisi** yaeleza chanzo kifo cha padri

UKURASA 4




# Mauaji yatikisa

• **Bibi** adaiwa kuua wajukuu, ajuza auawa kwa kitu chenye ncha kali, mganga mbaroni madai kuua mtoto, kigogo CCM naye... *Endelea ukurasa 2*



Rais Samia Suluhu Hassan akizungumza na Mwandaaji wa filamu ya Royal Tour, ambaye pia ni mwandishi wa habari maarufu duniani, Peter Greenberg, walipokuwa wakijibu maswali ya wageni mashuhuri waliohudhuria uzinduzi wa filamu hiyo katika ukumbi wa Guggenheim Museum, New York, Marekani juzi. **PICHA: IKULU**

## Samia asimulia milima, mabonde kufanikisha filamu Royal Tour

UKURASA 3



## CAG aibua utata TANROADS ununuzi wa mtambo wa sukari

UKURASA 2


MICHEZO HERSI AFUNGUKA YA AUCHO UK.24

MAONI, KATUNI UK.6



Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba (kushoto), akizungumza na Makamu wa Rais wa Benki ya Dunia (anayesimamia nchi za Kanda ya Mashariki na Kusini mwa Afrika), Dk. Hafez Ghanem, wakati wa Mikutano ya Kipupwe ya Benki hiyo na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF), inayoendelea jijini Washington DC, Marekani, juzi. **PICHA: WFM**

# Mauaji yatikisa kila kona

**Na Waandishi Wetu**

WATU sita wameuawa katika matukio tofauti ya kikatili likiwamo la Katibu Mwenezi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Bariadi, kudaiwa kumuua mkewe kwa kumnyonga hadi kufa kwa kile kinachodaiwa kukataa kuhamia kanisa analosali mume wake.

Matukio hayo yametokea kwa nyakati tofauti ndani ya wiki moja, pamoja na tukio la bibi kumuua mjukuu na kumjeruhi mwingine kwa madai wanajisaidia ovyo, huku binti aliyehitimu darasa la saba mwaka jana, kutupa mtoto wa wiki tatu kwenye shimo la choo.

Kutokana na mauaji hayo, Jeshi Polisi Mkoa wa Simiyu, linamshikilia Katibu Mwenezi huyo, Alex Lukumambaga, kwa tuhuma za kumuua mke wake, Ernestina Bruno siku ya Jumapili ya matawi. Ernestina alizikwa alhamisi iliyopita.

Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Simiyu, Shedrack Masija, alisema mtuhumiwa huyo alikamatwa jana akiwa nyumbani kwake kata ya Ngulyati, Halmashauri ya Mji wa Bariadi, wakati uchunguzi ukiendelea kutokana na kelele nyingi za wananchi kuwa amemuua mkewe.

"Tumeamua kumkamata na kumuweka ndani Katibu Mwenezi huyo, ili kuruhusu uchunguzi ufanyike. Si unajua sisi Tanzania hatuna desturi ya kuchunguza huku mtuhumiwa akiwa nje? Ndiyo maana tunamshikilia," alisema Masija.

Masija alisema mtuhumiwa anadai kuwa alimpiga na kumnyonga mkewe baada ya kukuta ameweka tawi alilotoka nalo kanisani (siku hiyo ikiwa Jumapili ya Matawi).

"Alimpiga kwa kuwa alishamzuia kwenda kusali kanisani huko na sababu ya kumzuia ni baada ya mkewe kukataa kubadili dhehebu na kuhamia anakosali yeye," alisema baadhi ya majirani ambao majina yao yamehifadhiwa, waliotoa taarifa hiyo kuhusu chanzo cha mgogoro hadi kusababisha mauti.

**MGANGA AMCHINJA MTOTO**

Mtoto wa miaka miwili, Ivan Coloman, Mkazi wa Kijiji cha Ngumbaro, Kata ya Songu, wilayani Siha mkoani Kilimanjaro, anadaiwa ameuawa kwa kuchinjwa shingoni kwa panga na kisha kufichwa kwenye mfuko wa sandarusi na mtu anayedaiwa kuwa mganga wa kienyeji.

Baada ya kutekeleza ukatili huo, mtuhumiwa wa mauaji hayo, Jumanne Athuman (63), naye aliuawa muda mfupi baadaye kwa kushambuliwa na wananchi waliochukizwa na kitendo hicho.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kilimanjaro, Simon Maigwa, alisema mauaji hayo yalifanyika Aprili 18, mwaka huu, majira ya saa 8:00 mchana huko katika kijiji cha Ngumbaru.

"Ni kweli aliyemchinja mtoto na yeye ameuawa na wananchi wenye hasira. Lakini mpaka ninavyoongea, nimeshatuma kikosi kazi maalum kwenda Siha kufanya uchunguzi wa kina na wanileteе majibu,"alisema

Akizungumzia tukio hilo, shuhuda wa tukio hilo Julius Gasper, ambaye ni ndugu wa marehemu, alisema yeye akiwa nyumbani, watoto wanne walikuwa wanacheza nje, lakini baada ya muda kupita wakaonekana wakiwa watatu na alipowauliza yuko wapi mwenzao, wakasema wao hawajui alipoenda.

Kwa mujibu wa Gasper, baada ya taarifa hiyo, alichukua jukumu la kuanza kufuatilia aliko mtoto huyo na alipofika kwa jirani yao (Jumanne Athuman), waliona kiatu kimoja cha mtoto huyo (Ivan), kikiwa mlangoni, huku mlango ukiwa umefungwa na damu zikichuruzika kutoka ndani.

**BIBI ADAIWA KUUA MJUKUU**

JESHI la Polisi mkoani Shinyanga, linamshikilia, Tatu Moshi (45) mkazi wa Lyabukande wilayani Shinyanga, kwa tuhuma za mauaji ya mjukuu wake, Joseph Juma (4), baada ya kumpiga sehemu mbalimbali za mwili wake na kumwagia maji ya moto, huku akimjeruhi mwingine mwenye umri wa mwaka mmoja na miezi saba kwa madai wanajisaidia ovyo ndani ya nyumba.

Kamanda wa Polisi mkoani Shinyanga, George Kyando, alibainisha hayo jana wakati akizungumza na vyombo vya habari na kusema kuwa tukio hilo lilitokea juzi majira ya asubuhi.

Alisema mwanamke huyo amekuwa na tabia ya kupiga wajukuu zake mara kwa mara, kwa madai kuwa wanatabia ya kujisaidia hovyo.

Kyando alisema katika tukio la siku hiyo, mtuhumiwa huyo alimpiga mjukuu wake sehemu mbaya za mwili na kusababisha kifo chake, huku mjukuu mwingine, Jimmy Lameck mwenyewe akijeruhiwa.

"Jeshi la Polisi mkoani Shinyanga tunamshikilia mwanamke, Tatu Moshi kwa tuhuma za mauaji ya mjukuu wake, pamoja na mama mzazi wa mtoto huyu Herena Nicolaus, ambaye amekuwa akishuhudia vipigo hivyo na hatoi taarifa juu ya ukatili ambao wanafanyiwa watoto wake na bibi yao," alisema Kyando.

"Chanzo za mauaji haya ni bibi wa watoto hawa kudai kuwa wajukuu zake wamekuwa na tabia ya kujisaidia hovyo, ndipo akaamua kuwa anawapiga, ili waache tabia hiyo na kusababisha mauaji ya mjukuu wake mmoja baada ya kumpiga vibaya na kumwagia maji ya moto," aliongeza.

**AUAWA KIKATILI**

Mkazi wa Mtaa wa Mpanda Hoteli katika Manispaa ya Mpanda mkoani Katavi, Marieta Thomas (90), ameuawa kwa kuchomwa na kitu chenye ncha kali kichwani na watu wasiojulikana.

Akizungumza na Nipashe, mjukuu wa bibi huyo, Rosemary Titus, amesema bibi yake ameuliwa jana akiwa nyumbani kwake.

Alisema bibi yake alikuwa anaishi mwenyewe na wao walikuwa wakimpelekea mahitaji pale anapohitaji huduma.

"Nimepigiwa simu na dada yangu leo asubuhi akaniambia bibi ameuliwa, nilishtuka sana, nimekuja nimekuta wamemuua, ingawa hakuna mgogoro wowote uliokuwapo," alisema Rosemary.

Peter Mwita, jirani wa bibi huyo, alisema alimuona bibi huyo siku moja kabla ya kifo chake na hakuwa na tatizo lolote.

"Jana jioni kabla sijaenda lindoni nilipita, alikuwa amekaa hapa nje, nikamsalimia, nashangaa kusikia ameuawa ila wachunguze labda kutakuwa na mgogoro wa kifamilia," alisema jirani huyo.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Mpanda Hoteli, Christina Ibrahimu, alikiri kutokea kwa tukio hilo baada ya kupigiwa simu na mwananchi wake na kuambiwa kwenye eneo lake yametokea mauaji ya bibi huyo.

Kamanda wa Polisi mkoa wa Katavi, Ali Makame, alisema upelelezi wa awali unaonyesha tukio hilo linahusishwa na imani za kishirikina.

**TAKWIMU MATUKIO UKATILI**

Matukio hayo yametokea ikiwa ni siku chache tangu Aprili 6, mwaka huu, Waziri wa Mambo ya Ndani, Hamad Masauni, alipotoa bungeni takwimu za matukio ya ukatili yaliyoripotiwa vituo vya polisi tangu mwaka 2019 hadi Machi mwaka huu.

Alisema matukio ya ubakaji yaliyoripotiwa kwa kipindi hicho ni 19,726 na matukio ya kulawiti ni 3,260, na kwamba kesi zilizofikishwa mahakamani ni 21,063 ambapo washtakiwa 14,278 walihukumiwa.

**Imeandikwa na Happy Severine (BARIADI), Anjela Mhando (SIHA), Marco Maduhu (SHINYANGA) na Neema Hussein (KATAVI),**

# Utata waibuliwa TANROADS kununua mtambo wa sukari

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

MDHIBITI na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) amebaini kusuasua kwa utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa Kiwanda cha Sukari Mkulazi mkoani Morogoro.

Vilevile, amebaini kukosekana kwa uwazi katika mchakato wa ununuzi wa mtambo wa kuzalisha sukari kwa ajili ya kiwanda hicho na utata wa Wakala wa Barabara (TANROADS) kupewa zabuni ya kununua na kufunga mtambo huo.

CAG Charles Kichere ametoa angalizo la kutokea hasara katika uwekezaji huo unaotumia fedha za wanachama wa Shirika la Hifadhi ya Jamii (NSSF) katika ripoti yake ya ukaguzi kwa mwaka 2020/21 ambayo sasa iko wazi kwa umma baada ya kuwasilishwa bungeni wiki iliyopita.

Anafafanua kuwa Mkulazi ni kampuni tanzu ya NSSF (kwa asilimia 96) na Shirika la Magereza (asilimia nne) inayotekeleza miradi miwili ya viwanda vya sukari (eneo la Mkulazi na Mbigiri) vinavyolenga kuzalisha tani 250,000 za sukari kwa mwaka.

Anasema kwa mujibu wa Mpangomkakati wa Kampuni ya Mkulazi (2020/21 -2025/26) uliofanyiwa marekebisho, mradi wa Mbigiri ulitarajiwa kuanza uzalishaji msimu wa mwaka 2021 na kuzalisha tani 15,234 za sukari ifikapo msimu wa mwaka 2022.

"Mradi wa Mkulazi ulipanga kuanza uzalishaji katika msimu wa mwaka 2023 kwa makadirio ya uzalishaji wa tani 31,098 za sukari ifikapo msimu wa 2024.

"Hata hivyo, katika ukaguzi wangu, nilibaini hadi tarehe 26 Februari 2022, Kampuni ya Mkulazi ilikuwa haijakamilisha ufungaji wa mashine za kiwanda katika eneo la Mbigiri ambapo ujenzi ulikuwa umefikia asilimia 13.8 na ujenzi wa miundombinu ya eneo la Mkulazi ulikuwa unaendelea.

"Kampuni ya Mkulazi ilinieleza kuwa kucheleweshwa kwa ufungaji wa mashine kiwandani kulisababishwa na mlipuko wa janga la UVIKO-19 lililoathiri kuwasili kwa mashine zilizonunuliwa nje ya nchi na kusafiri kwa washauri wa ufungaji wa kiwanda," anasema.

Vilevile, CAG alibaini kuwa kutokana na kuchelewa kwa ujenzi na ufungaji wa mashine za kiwanda cha sukari, Kampuni ya Mkulazi iliuza miwa iliyovunwa kwa sababu kiwanda hakikukamilika ili kuanza uzalishaji wa sukari.

Anabainisha kuwa kwa mwaka wa fedha 2020/21, kampuni ilivuna hekta 382 za miwa na kuuza tani 32,121.6 kwa Sh. bilioni 1.16.

**UTATA UNUNUZI MTAMBO**

CAG pia anabainisha kuwapo udhaifu katika ununuzi wa mtambo wa kiwanda cha sukari katika Kampuni ya Mkulazi Holding Company Limited.

Anasema udhaifu huo unajumuisha ukosefu wa sababu za msingi za kuihusisha TANROADS katika ununuzi wa mtambo wa kiwanda hicho cha sukari.

CAG anaendelea kubainisha kuwa Menejimenti ya Kampuni ya Mkulazi haikutoa sababu za msingi za kuchagua TANROADS kufanya ununuzi kwa niaba yake na siyo taasisi zenye uzoefu wa ununuzi kwa niaba ya taasisi za serikali kama vile TEMESA au Wakala wa Ununuzi Serikalini.

"Pia nilibaini Kampuni ya Mkulazi haikutekeleza wajibu wake wa ununuzi kama ilivyokuwa imeelezwa kwenye makubaliano. Kwa mujibu wa nakubaliano, TANROADS alitakiwa kufanya mchakato wa ununuzi hadi zabuni itakapotolewa kwa mshindi wa zabuni na utiaji saini ulipaswa kufanywa na Kampuni ya Mkulazi.

"Hata hivyo, nilibaini kuwa TANROADS ilifanya mchakato mzima wa ununuzi. Hapakuwa na ushahidi kuwa Kampuni ya Mkulazi ilihusika katika kuandaa mahitaji, vipimo na makadirio ya majenzi (BOQ) kwa ajili ya kusanifu, kuleta, kusimika na kuuzindua mtambo wa kiwanda cha sukari (pamoja na kusafisha) kabla ya mwaliko wa zabuni kama ilivyoainishwa katika makubaliano," anafafanua.

**UDHAIFU UTIAJI SAINI**

CAG anasema kuwa wakati makubaliano yaliitaka Mkulazi kutia saini mkataba, alibaini kuwa makubaliano hayo yalifanyiwa marekebisho ili kuipa TANROADS mamlaka ya kutia saini.

Anabainisha zaidi kuwa Oktoba 23, 2019, TANROADS iliingia mkataba wa usanifu, kuleta, kuusimika na kuzindua mtambo wa kiwanda kwa bei ya mkataba ya dola za Marekani milioni 50.86 na Sh. bilioni 11.74 cha ziada ikiwa ni pamoja na kodi nyinginezo za ndani.

"Sikupata ushahidi kuwa mkataba ulihakikiwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali kama inavyotakiwa na Kanuni ya 59(1) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2013.

"Aidha, Kampuni ya Mkulazi haikuwa na jukumu la kusimamia huo mkataba na hivyo mradi unasimamiwa na TANROADS. Kwa hivyo, malipo kwa ajili hiyo hufanywa na NSSF baada ya kupokea hati na nyaraka za malipo kutoka TANROADS.

HABARI KITAIFA

# ... Wabunge wammwagia pongezi, wapewa somo kuhusu makadirio wizara ya utalii

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

BUNGE limempongeza Rais Samia Suluhu Hassan anavyoendelea kutangaza utalii kupitia filamu maalum ya The Royal Tour huku wabunge wakitakiwa kufuatilia kwa umakini ili wakati wa makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii, watoe michango yao.

Spika wa Bunge, Dk.Tulia Ackson alitoa kauli hiyo bungeni jana mara baada ya kumalizika kwa kipindi cha maswali na majibu huku akisema filamu hiyo ina lengo la kuitangaza Tanzania na vivutio vilivyopo hatua ambayo itaongeza watalii nchini.

"Sisi sote tunatambua jana Mheshimiwa Rais Samia amezindua filamu maalum ya kuhamasisha utalii nchini, kwa sababu waheshimiwa wabunge huwa mnachangia sana kuhusu kuongeza idadi ya watalii wanaokuja.

"Kwa niaba yenu wote sisi kama Bunge tunampongeza kwa hatua anayochukua kwenye hili eneo la kuongeza watalii. Kwa hiyo waheshimiwa wabunge kwa sababu bajeti ya Maliasili na Utalii inakuja hivi karibuni, ni muhimu sana kila mbunge afuatilie mambo yanayoendelea huko ili kama kuna la kuishauri hapa na pale itakuwa rahisi,"alisema.

Alisema lengo la kufuatilia ni kujua hatua zilizochukuliwa na zile wanazotamani ziongezeke.

Akizungumza nje ya Bunge, Mbunge wa Viti Maalum (CHADEMA), Esther Matiko, alimpongeza Rais kwa kuwa na utashi wa kisiasa kuhakikisha anautangaza utalii wa Tanzania ambao takwimu za serikali zinaonyesha unachangia asilimia 25 ya fedha za kigeni na asilimia 17.5 ya pato la taifa.

Matiko alishauri serikali kuwekeza kwenye utalii wa michezo kwa kujenga viwanja vya kisasa vya michezo mbalimbali; utalii wa matibabu kwa kujenga hospitali za kisasa na kumbi za mikutano ili ifanyike mikutano ya kimataifa nchini.

"Tangu tupate uhuru hatujawahi kupata watalii milioni mbili tofauti na nchi zingine wanatengeneza 'artificial' utalii (utalii bandia). Wanapata watalii zaidi ya watalii milioni nne au nane.

"Kwa kuwa ameonyesha huu utayari tuangaze na eneo lingine utalii wa kimatibabu tutapata wateja wengi kuja Tanzania, utalii wa kimichezo kwa kujenga viwanja kwa mfano kwenye mpira wa kikapu wanaenda Rwanda. Tuandae mikutano ya kimataifa, hoteli zitapata watu. Hii ni nzuri sana Tanzania imetangazika, nimshauri Rais aweke ze na huko ikiwezekana tuandae hata Kombe la Dunia," alisema.

Mbunge wa Hai (CCM), Saashisha Mafuwe, alisema matokeo ya filamu hiyo yataonekana haraka kwenye uchumi wa nchi kwa kuwa sekta ya utalii imekuwa na mchango mkubwa kwenye pato la taifa.

"Ni wajibu wetu Watanzania kuunga mkono jitihada hizi kubwa ili wageni watakapokuja wakutane na mazingira rafiki na kwamba wananchi wa jimbo la Hai tayari wamejiandaa kikamilifu kuwapokea wageni ikizingatiwa ni wadau wakubwa wa utalii kwani Mlima Kilimanjaro upo kwenye jimbo langu," alisema.

Naye Mbunge wa Kigamboni (CCM), Dk.Faustine Ndugulile, alisema filamu hiyo imelenga kutangaza utalii wa Tanzania na itaonyeshwa Marekani na Ulaya.

Mbunge wa Mpanda Mjini (CCM), Sebastian Kapufi, aliwataka Watanzania kumuunga mkono Rais kwa sababu imekuwa kilio cha muda mrefu cha kupata jukwaa la kuutangaza utalii wa nchi kwa kina.

Mbunge wa Makete(CCM), Festo Sanga alisema filamu hiyo ni ya kihistoria ya kuupeleka utalii kwenye dunia ya watalii na kuitaka wizara husika kujiandaa kuweka mazingira mazuri ya watalii kuishi na kuhudumiwa ndani ya hifadhi zilizopo nchini.

Alitaka kuwapo na ushirikishwaji wa sekta binafsi na uwe wa hali ya juu kwa wale wanaojihusisha na utalii.

Mbunge wa Kuteuliwa, Riziki Lulida, alisema Tanzania lazima itangazwe kupitia filamu ya Royal Tour na kwamba hatua hiyo imezindua dunia kujua utalii uliopo nchini ikiwamo Serengeti, Mlima Kilimanjaro na maeneo mengine ambayo nchi zingine zimekuwa zikidai ni yao. Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Maliasili, Ally Makoa, alisema hatua ya Rais ya kuutangaza utalii italeta mchango mkubwa kwenye sekta hiyo kwa kutambulisha nchi na kuongeza idadi ya watalii na watanzania watapata ajira.

Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti, Omary Kigua, alisema Samia ni Rais wa kwanza kufanya jambo kubwa la aina hiyo na kwamba nchi itakwenda kupata maendeleo kutokana na mapato ya nchi kuongezeka.




Mwendesha pikipiki, akipita jirani na chemba ya majitaka iliyoziba na kutiririsha maji machafu katika Mtaa wa Moyo, Mikocheni, mkoani Dar es Salaam jana na kusababisha harufu mbaya na kero kwa wakazi wa eneo hilo. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Samia aeleza milima, mabonde kufanikisha filamu Royal Tour

**Na Jenifer Gilla**

RAIS Samia Suluhu Hassan, jana alieleza aliyopitia wakati wa kurekodi filamu ya Royal Tour, ikiwamo kuendesha gari la mfumo wa kawaida (manual) kwa mara ya kwanza baada ya miaka 15.

Lingine ni kuwa na waongoza watalii wengi ambao walikuwa wakimwelekeza vitu vya kufanya, yakiwamo maeneo anayotakiwa kwenda na asiyotakiwa.

Rais aliyasema hayo jana alipokuwa akijibu maswali ya wadau wa utalii na sanaa baada ya uzinduzi wa filamu ya hiyo, uliofanyika katika jumba la Makumbusho la Guggenheim, New York, Marekani, yaliyoongozwa na mwandishi wa habari nguli nchini humo, Peter Greenberg.

Katika mahojiano hayo mwanahabari huyo alimwuliza Rais kama ni mara yake ya kwanza kuendesha gari mwenyewe kwa muda mrefu naye akajibu: "Baada ya miaka 15, ndiyo."

Rais Samia alisema kitu kilichomfurahisha zaidi wakati wa utengenezaji wa filamu hiyo ni kuongoza shughuli za utalii, ingawa alikiri kuwa haikuwa kazi rahisi kutokana na kuzungukwa na waongoza utalii wengi ambao walikuwa wakimwelekeza vitu vya kufanya.

"Nilikuwa na waelekezaji wengi ambao walikuwa wakiniambia usifanye hiki, usifanye kile, usiende pale, lakini ilinibidi niendelee na kazi. Hivyo ndivyo ilivyokuwa na nilifanikiwa," alisema huku akitabasamu.

Alisema pia hakutarajia kama filamu hiyo ingetoka katika ubora mzuri kwa sababu ilirekodiwa sehemu tofauti huku mtangazaji huyo akisema ilikuwa ikirekodiwa kwa saa 14 hadi 15 kwa siku, hivyo hawakupata muda mzuri wa kulala na wakati mwingine iliwalazimu kula mlo mmoja au miwili kutokana na kutingwa na kazi.

Akijibu swali la Greenberg ambaye pia ndiye aliyeandaa filamu hiyo kuhusu ni kitu gani wageni wakitegemee wanapokwenda kutembelea Tanzania, Rais Samia alisema Watanzania ni wakarimu, hivyo wageni watakaotembelea nchi watafurahia hilo.

Pia Rais alisema ana mpango wa kuwaunganisha waigizaji wa Tanzania na dunia ikiwa ni moja ya mikakati ya kuitangaza nchi pamoja na vivutio vyake duniani.

Alisema hivyo wakati akijibu swali kutoka kwa msichana wa Kitanzania anayeishi Marekani aliyejitambulisha kwa jina la Maria, aliyetaka kufahamu mpango wa nchi katika kusaidia wasanii wadogo wenye malengo ya kuendeleza kile ambacho nchi imeakianzisha.

"Kwa mwigizaji mdogo wa kike ambaye najivunia sana nchi yangu, ni kitu gani serikali yangu itatoa kuendeleza kile ulichoanzisha, ambacho ni kizuri, kuendeleza kuionyesha nchi yangu, kuendeleza kufuata nyayo zako kuionyesha dunia ni kwa namna gani Tanzania ni sehemu nzuri?" aliuliza Maria.

Akijibu swali hilo, Rais Samia alisema ameazimia kuunganisha waigizaji wa Tanzania na kuwa ameshaanza kufanya mikutano na wadau wakubwa wa tasnia hiyo, hivyo wampe nafasi atatekeleza.

"Jana (juzi) nilikuwa na mkutano mzuri na taasisi tano kubwa katika sekta ya usafiri hapa Marekani. Kwa hiyo nilikuwa na mazungumzo mazuri nao. Na moja katika mazungumzo hayo, nilikutana na mtu ambaye anafanya kazi Paramount na IMC. Kwa hiyo tulikuwa na mazungumzo mazuri na kuunganisha utamaduni na sanaa ya Tanzania katika sekta hiyo. Hivyo nadhani nimeanza kuwafanyia kazi, nipe muda," alifafanua Rais.

Baada ya mazungumzo hayo, Greenberg ambaye alifurahia kusikia 'Big Five' (wanyama watano maarufu) katika nyanja nyingine baada ya ile ya wanyama iliyomo katika filamu ya Royal Tour, alisema leo watakuwa na mazungumzo zaidi yatakayohusu suala hilo la sanaa ya filamu.

Paramount Pictures ni moja ya kampuni kubwa tano za filamu duniani zikiwamo Gaumont Film ya Ufaransa iliyoanzishwa mwaka 1895, Pathé (1896), Titanus (1904), Nordisk Film (1906), na Universal Studios (1912).

Rais Samia aliondoka nchini wiki iliyopita kwenda Marekani ambako pamoja na mambo mengine, alizindua filamu iliyojumuisha wadau takribani 400 wa tasnia za utalii, sanaa, burudani na uwekezaji.

HABARI KITAIFA

# Polisi yaeleza sababu kifo cha Padri

**Na Romana Mallya**

JESHI la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, limesema limekamilisha uchunguzi wa mwili wa Padre wa Parokia ya Mbezi Mshikamano, Francis Kangwa, ambao unaonyesha kuwa na dalili za kujiua.

Mwili wa Padre huyo ulikutwa ndani ya tangi la kuhifadhia maji jirani ya nyumba ya mapadre wa Shirika la Wamisionari wa Afrika, Posta jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na Nipashe jana Kamanda wa kanda hiyo, Jumanne Muliro, alisema Jeshi la Polisi limekamilisha uchunguzi wa mwili huo na kwa sasa linapeleleza sababu za kujiua.

"Kuna dalili kubwa za yeye kujiua, kwa nini amejiua ndiyo tunapeleleza. Eneo la tukio kuna tangi kubwa la maji na kuna ngazi, alivua shati tu. Uchunguzi wa mwili huo umeshakamilishwa na kifo chake kimetokana na kukosa hewa," alisema.

Mmoja wa waumini katika kanisa hilo ambaye hakutaka jina lake liandikwe gazetini alisema Padre huyo hakuwa mtu mbaya.

"Aliishi vizuri na watu na ndiyo maana waumini tunatamani kujua shida ni nini? Jambo gani limetokea? Alikuwa mtu wa watu kwa waumini, watoto, wenye umri wa kati, wazee alikuwa mtu mzuri, alikuwa anaweza kukushauri kwa nini ukae karibu na Mungu, uabudu na utende mambo mazuri duniani," alisema.

Mwili wa Padre huyo unatarajia kuzikwa kesho katika makaburi ya mapadre Pugu, jijini Dar es Salaam.

Taarifa ya kifo chake ilitangazwa kwa mara ya kwanza Ijumaa Kuu na Paroko Msaidizi, Padre Louis Mtamati.

Aprili 12, mwaka huu, Padre huyo aliegeza gari lake kwenye nyumba ya mapadre wa shirika hilo ya Atiman House eneo la Posta na kuhudhuria ibada ya kubariki mafuta ya Crism ndani ya Kanisa Kuu la Mtakatifu Joseph na baadaye kula chakula cha mchana na wenzake.

Siku iliyofuata hakuonekana wala kupatikana katika simu yake ya kiganjani huku gari lake likiwa kwenye maegesho Atiman House na wakati wakijiandaa kutoa taarifa polisi ndipo mwili wake ulipobainika kuwapo ndani ya tangi la maji.



Meneja Usimamizi wa kampuni ya Tawakal inayotoa huduma za mabasi kati ya Tanzania na Kenya, Athumani Abdarahaman, akizungumza na waandishi wa habari jijini Tanga jana, akiiomba serikali ipitie haraka mchakato wa kuongeza nauli kutokana na kupanda kwa bei za mafuta **PICHA: BONIFACE GIDEON**

## Kichanga cha wiki tatu chakutwa shimo la choo

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

MTOTO anayesadikiwa kuwa na umri wa wiki tatu, ameokotwa kwenye shimo la choo cha Shule ya Msingi Magindu, wilayani Kibaha baada ya kutupwa na mama yake.

Akizungumza na Nipashe jana, Diwani wa Magindu, Erasto Makala, alisema mtoto huyo alikutwa kwenye shimo hilo usiku wa kuamkia jana.

Makala alisema mama wa mtoto huyo, anayejulikana kwa jina la Belita, baada ya kumtumbukiza mtoto huyo chooni anadaiwa kukimbilia kusikojulikana.

Alisema kwa sasa wanawasiliana na watu wa ustawi wa jamii kwa ajili ya kumchukua mtoto huyo na kwamba bibi wa mtoto huyo amemtambua mjukuu wake na sasa anashikiliwa na polisi kwa ajili ya mahojiano.

Kaimu Ofisa Mtendaji wa Kata ya Magindu, Shabani Muhidini, alikiri kuokotwa mtoto huyo majira ya saa 9:00 usiku wa kuamkia jana.

Muhidini alisema mlinzi wa shule ndiye aliyesikia sauti ya mtoto akilia kwenye shimo la choo, hivyo kwenda kuwaamsha walimu walioko karibu wakabomoa shimo na kumtoa mtoto huyo akiwa hai.

"Mlinzi baada ya kusikia sauti ya mtoto kutoka chooni aliwaamsha walimu wakatumia tochi kumulika na walimwona mtoto huyo akiwa hai," alisema Muhidini.

Alisema mtoto huyo aliokolewa na alipelekwa kupata huduma ya kwanza katika Kituo cha Afya Magindu na sasa anaendelea vizuri.

"Baada ya kushirikiana na wenyeviti kutambua ni nani amejifungua hivi karibuni, akatambulika kuwa aliyemtupa mtoto ni mtoto wa Belita ambaye alihitimu darasa la saba mwaka 2021. Alipotafutwa hakupatikana alikuwa tayari ametoroka," alisema.

Mtendaji huyo alisema wazazi wa binti aliyetupa mtoto, walipoulizwa kuhusiana na mtoto wao hawakuweka wazi sababu za binti yao kufanya tukio hilo ingawa wako baadhi ya majirani waliosema hakukuwa na maelewano mazuri kati ya binti huyo na wazazi wake tangu alipogundulika kuwa mjamzito.

Muhidini alisema kuna taarifa za kupatikana kwa binti huyo maeneo ya Mbezi akijaribu kutoroka na taratibu za kurudishwa polisi Mlandizi kwa hatua za kisheria zinaendelea.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Pwani, Pius Lutumo, alipoulizwa kuhusiana na tukio hilo alisema bado hajapata taarifa.

# CAG ashtukia vikwazo viwili uwekezaji nchini

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

MDHIBITI na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), ametaja mambo mawili yanayokwaza uwekezaji nchini, huku Tanzania ikishika nafasi ya 14 kati ya 190 kwenye orodha ya nchi zenye mazingira rafiki kwa uwekezaji.

Katika ripoti yake ya ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2020/21 iliyowasilishwa bungeni jijini hapa Jumanne ya wiki iliyopita, CAG Charles Kichere anasema mazingira yasiyoridhisha ya uwekezaji ni miongoni mwa vikwazo vinavyoyakabili mataifa yanayoendelea.

Anasema marekebisho ya kimfumo mara nyingi ni suala muhimu la kuondoa vizuizi vya uwekezaji, akirejea ripoti inayoitwa 'Easy of Doing Business Report, 2020' iliyotolewa na Shirika la Kimataifa la Fedha (International Finance Corporation), Tanzania ikiorodheshwa katika nafasi ya 141 kati ya nchi 190.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, kwa miaka mitano iliyopita, kuanzia mwaka 2015 hadi 2020, Tanzania ilishuka kwa asilimia nane (8) katika kuwekeza mazingira rafiki ya biashara.

"Nafasi hii iko chini ya makadirio ya nchi ya kuwamo kwenye nafasi 100 za juu ifikapo mwaka 2020 kama ilivyoainishwa katika Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano - II (2016/17-2020/21).

"Tanzania inafanya jitihada mbalimbali ili kuboresha mazingira ya uwekezaji nchini. Hata hivyo, katika mapitio yangu ya shughuli za Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), nilibaini upungufu unaoathiri mazingira ya uwekezaji nchini," anabainisha.

CAG anataja mambo mawili aliyoyabaini kukwaza uwekezaji nchini, yakijumuisha matumizi duni ya majukwaa ya mtandao ili kukuza uwekezaji.

Anafafanua kuwa mapitio ya taarifa za mipango ya TIC katika kukuza fursa za uwekezaji kupitia majukwaa ya mtandaoni yalibaini kituo hakitumii majukwaa ya mitandao kikamilifu.

"Kituo kilikuwa kimetoa makala moja tu ya video ya uhamasishaji wa uwekezaji kwa lugha ya Kiswahili pekee iliyotolewa mwezi Novemba 2017; pia kituo hakikuweka kwenye mtandao mkataba wa huduma kwa mteja kwenye Dirisha la Uwekezaji Tanzania kwa ajili ya uelewa kwa wadau.

"Kituo hakikuchapisha kwenye tovuti yake mwongozo wa huduma za vibali, leseni na mahitaji ya usajili. Nina maoni kuwa utumiaji bora wa majukwaa ya kimtandao una athari chanya kubwa katika kukuza uwekezaji nchini.

"Ninapendekeza TIC iongeze matumizi ya majukwaa ya mitandao kwa kushirikiana na wadau wengine ili kukuza uwekezaji nchini," CAG Kichere anawasilisha hoja yake.

Analitaja jambo la pili linalokwaza uwekezaji ni vikwazo katika kutoa motisha na vivutio kwa wawekezaji wa kimkakati.

CAG anafafanua kuwa vifungu vya 19 na 20 vya Sheria ya Uwekezaji Tanzania, Sura ya 38 (kama ilivyorekebishwa mwaka 2015) kupitia vifungu vya 19 na 20 vya Sheria ya Fedha za Umma ya Mwaka 2015, vinaruhusu kutoa motisha maalum kwa uwekezaji wa kimkakati na uwekezaji mkubwa kwa agizo lililochapishwa kwenye Gazeti la Serikali linalotolewa na Waziri wa Fedha na Mipango kufuatia mapendekezo ya Kamati ya Kitaifa ya Uwekezaji.

"Nilipitia motisha maalum na vivutio vilivyotolewa kwa wawekezaji kufikia tarehe 30 Juni 2021 na nikabaini miradi 19 iliyoidhinishwa na Kamati ya Kitaifa ya Uwekezaji kupewa motisha na vivutio vya ziada kuanzia mwaka 2015 ilikuwa haijachapishwa kwenye Gazeti la Serikali ili kukamilisha na kuhalalisha utoaji wa motisha husika.

"Hali hii imesababisha utoaji wa motisha na vivutio vya ziada kuchelewa kwa miaka sita. Pia nilibaini kuwa wawekezaji sita (6) walikuwa hawapata majibu ya maombi yao ya kupewa motisha na manufaa ya ziada toka Juni 2020 hadi wakati wa ukaguzi huu mwezi Novemba 2021.

"TIC ilieleza kuwa Waziri wa Fedha na Mipango amewekewa ukomo na sheria kuu za kodi (Sheria ya Kodi ya Mapato na Kodi ya Ongezeko la Thamani) juu ya utoaji wa motisha na vivutio vya ziada vya uwekezaji wa kimkakati na uwekezaji mkubwa zaidi ya vile vinavyoruhusiwa kisheria. TIC inapanga kuwasilisha ombi la marekebisho ya sheria hizo.

**HABARI KITAIFA**

## Dada, kaka kortini kwa tuhuma kuuza dawa za kulevya

**Na Jumbe Ismailly,** IGUNGA

WATU wawili wa familia moja, wakazi wa Mtaa wa Kamando,Kata ya Igunga mkoani Tabora Mjini, Caroline Isack (35) na kaka yake Brayson Isack (30), wamepandishwa kizimbani katika Mahakama ya Hakimu Mfawidhi Wilaya ya Igunga kwa tuhuma za kuuza dawa za kulevya.

Dawa hizo zinasadikiwa ni bangi yenye uzito wa gramu tano na heroine yenye uzito wa gramu 1.6.

Mwendesha Mashtaka, Elimajid Kweyamba, alidai kwamba tukio hilo lilitokea Desemba,16,mwaka 2021 majira ya usiku katika Mtaa wa Kamando na kwamba watuhumiwa hao walikutwa wakiuza dawa hizo .

Mbele ya Hakimu Mfawidhi wa Mahakama ya Wilaya ya Igunga, Lydia Ilunda, Kweyamba alidai kuwa siku ya tukio, washitakiwa walikamatwa na maofisa wa polisi wakiuza dawa hizo.

Alidai pia kwamba washitakiwa walitenda makosa hayo mawili kinyume na kifungu cha 17 kifungu kidogo cha kwanza (a) (2) cha Sheria ya Kuzuia Dawa ya Kulevya sura ya No. 95 kama ilivyofanyiwa mapitio mwaka 2019.

, Kweyemba alidai kwamba upelelezi wa kesi hiyo umekamilika na kuomba tarehe nyingine kwa ajili ya usikilizwaji wa maelezo ya awali.

Hata hivyo, baada ya kusomewa mashitaka hayo, washitakiwa walikana, hivyo kesi hiyo imeahirishwa hadi Aprili 28, mwaka huu na watuhumiwa wapo nje kwa dhamana ya Shilingi milioni tano kila mmoja.

**Mwendesha Mashtaka, Elimajid Kweyamba, alidai kwamba tukio hilo lilitokea Desemba,16,mwaka 2021 majira ya usiku katika Mtaa wa Kamando na kwamba watuhumiwa hao walikutwa wakiuza dawa hizo**

# Benki ya Dunia yaahidi kuisaidia Tanzania

**Na Benny Mwaipaja,** WASHINGTON DC

BENKI ya Dunia imekubali kuisaidia Tanzania kukabiliana na athari za kiuchumi zinazotokana na madhara ya UVIKO-19 na vita vinavyoendelea kati ya Russia na Ukraine, huku Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, akiishukuru.

Waziri Nchemba alitoa shukrani hizo baada ya kukutana na kufanya mazungumzo na Makamu wa Rais wa Benki ya Dunia, anayesimamia nchi za Kanda ya Mashariki na Kusini mwa Afrika, Dk. Hafez Ghanem, wakati wa Mikutano ya Kipupwe ya Benki hiyo na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF), inayoendelea jijini Washington DC, Marekani.

Alimweleza kwamba Tanzania inafanya kila njia kuhakikisha kuwa uchumi wake ulioathiriwa na matukio hayo unarejea katika hali ya kawaida kwa kutafuta rasilimali fedha na kuzielekeza kwenye sekta zitakazochochea ukuaji wa uchumi ikiwamo kilimo, na kuimarisha sekta binafsi. 'Tumepokea taarifa ya namna Benki ya Dunia na Shirika la IMF linavyokusudia kufufua uchumi wetu kwa kuwekeza kwenye sekta za uzalishaji ikiwamo kilimo, mifugo na uvuvi pamoja na kuisaidia sekta binafsi hususan wajasiriamali wakiwemo wamachinga," alisema Dk. Nchemba.

Alisema Wizara ya Fedha na Mipango kwa kushirikiana na wataalam wa Benki ya Dunia, IMF na Benki ya Maendeleo ya Afrika, watakutana ili kupitia maeneo ambayo yanahitaji kufanyiwa kazi ili utekelezaji wa miradi hiyo ianze Mwaka mpya wa Fedha 2022/2023.

"Tuna maeneo yanayohitaji uangalizi wa karibu yakiwamo ya mfumuko wa bei, kupanda kwa bei za bidhaa ambayo ni muhimu kwa wananchi wetu na yanahitaji Serikali ipunguze kodi na fidia ya fedha hizo zinatakiwa zipatikane kutoka kwenye vyanzo vingine, kama tunavyoendelea na mijadala hii," aliongeza Waziri Nchemba.

Ghanem alipongeza mabadiliko makubwa ya kisera na kiuchumi yanayoendelea nchini, ambayo anaamini yatasaidia kukuza uchumi wa nchi na wananchi wake.

Aliahidi kuwa Benki yake itaisaidia Tanzania na nchi nyingine za Afrika kukabiliana na athari za majanga ya ugonjwa wa Uviko na athari za vita vya Ukraine na Russia vilivyosababisha kupanda kwa bei za bidhaa zikiwamo bei za mafuta na vyakula duniani kote.

Waziri Nchemba yuko Marekani akiongoza ujumbe wa Tanzania kwenye mikutano ya Kipupwe ya Benki ya Dunia na Shirika la Fedha la Kimataifa - IMF, ambayo imewakutanisha Magavana wa Taasisi hiyo, mashirika yasiyo ya kiserikali na sekta binafsi ambapo dhima kubwa ya mwaka huu ni kuchambua na kutoa mapendekezo ya namna ya kufufua uchumi wa nchi ulioathiriwa na matukio hayo.



Mafundi wakiwa katika ujenzi wa barabara ya mabasi yaendayo haraka katika barabara ya Kawawa, mkoani Dar es Salaam, jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Maslahi ya madiwani na wenyeviti yatikisa Bunge

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

SPIKA wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, ameagiza Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuifanyia kazi hoja ya maslahi ya madiwani na wenyeviti wa vijiji na vitongoji.

Alitoa agizo hilo bungeni jijini hapa jana wakati akiahirisha kikao cha mchana cha Bunge baada ya wabunge wengi waliochangia mjadala wa makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI kulalamika kuhusu maslahi ya madiwani na wenyeviti hao.

Wabunge waliochangia mjadala huo na kuligusia suala hilo ni pamoja na Deo Sanga (Makambako), Florent Kyombo (Nkenge), Mwita Getere (Bunda), Christina Ishengoma (Viti Maalum), Mussa Sima (Singida Mjini), Robert Maboto (Bunda Mjini), Noah Mollel (Arumeru Magharibi) na Ramadhani Ighondo (Singida Kaskazini), aliyetishia kushika shilingi ya waziri.

Spika Tulia alisema wabunge wengi wamelalamika kuhusu maslahi duni ya madiwani na wenyeviti wa vijiji na vitongoji, hivyo anaelekeza suala hilo liwe miongoni mwa hoja nyeti za kujadiliwa na Kamati ya Bajeti.

"Hoja hii ya maslahi ya madiwani, wenyeviti wa vijiji na vitongoji ichukuliwe na Kamati ya Bajeti na kuifanya kama moja ya hoja nyeti za kufanyiwa kazi," alisema.

Wabunge Robert Maboto (Bunda Mjini), Antony Mwantona (Rungwe), Njalu Silanga (Itilima) na Stanslaus Mabula (Nyamagana) waliitaka serikali kuongeza bajeti kwa ajili ya Wakala wa Barabara za Mjini na Vijijini (TARURA), wakisisitiza kuwa hali ya barabara hizo ni mbaya kwenye maeneo mengi nchini.

"Ni kweli bajeti ya TARURA imeongezwa hadi Sh. bilioni 800, lakini barabara zinazohitajika fedha ni nyingi. Kwenye Jimbo la Nyamagana pekee, kuna barabara zenye urefu wa zaidi ya Km 900 zinahitaji fedha," alisema Mabula.

Mbunge wa Urambo, Magreth Sitta (CCM), aliitaka serikali kuajiri walimu 600 wanaohitajika Urambo na kuungana na wabunge wenzake kutaka nyongeza ya posho za madiwani na kufikiria kuwa na utaratibu huo kwa wenyeviti wa vijiji na vitongoji.

Pia aliitaka serikali na wadau wa elimu kutoa huduma ya chakula kwa shule zote ili kuongeza ufaulu na kuimarisha afya za wanafunzi.

**VITI MAALUM**

Mbunge wa Viti Maalum, Juliana Shonza (CCM), alisema kutoshirikishwa kwa wabunge wa viti maalum katika kamati za fedha za halmashauri kumewafanya kushindwa kusimamia mikopo ya asilimia nne ya mapato ya halmashauri inayotolewa kwa wanawake.

Alisema wanawake wamewaamini kwenda kusimamia maslahi yao lakini katika vikao hivyo ambavyo vinajadili masuala yote ya fedha wabunge hao wamekuwa hawaingii.

"Fedha zinatolewa lakini hazirejeshwi, sisi ambao tunakaa na hao watu tunajua changamoto zao, hatushirikishwi katika vikao vya kamati za fedha," alilalamika.

Katika hilo, Spika wa Bunge, Dk.Tulia, alisema hoja hiyo imekuwa ikiibuliwa mara kwa mara bungeni lakini anafiriki ni muhimu kwa wabunge wanawake kukutana na kuwekana sawa kuhusu jambo hilo.

Alisema mbunge wa viti maalum anawakilisha halmashauri zote za mkoa wake na hawezi kuwa mjumbe wa kamati za fedha za halmashauri zote.

"Ndiyo maana ninasema lazima tukalizungumze kwa sababu wabunge wa majimbo wapo na wa viti maalum wapo, tunaweza kushauriana vizuri kuhusu jambo hili kuliko kufikiri ni jambo rahisi, " alisema.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Serikali isikilize kilio cha waagizaji magari

**HIVI** Karibuni, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alipotembelea Bandari ya Dar es Salaam, alisema magari yaliyotengenezwa chini ya mwaka 2010 yasiingizwe nchini, ili kuepusha nchi kuwa dampo.

Agizo hilo liliwaibua waagizaji na wauzaji wa magari wakiomba serikali ipunguze ushuru, ili Watanzania wengi wenye kipato cha kawaida waweze kuyaagiza matoleo mapya.

Wauzaji hao walisema wateja wao wamekuwa wakiagiza matoleo ya zamani kwa sababu ya bei zake kuwa chini, ambayo wana uwezo wa kuimudu ikilinganishwa na matoleo mapya.

Mathalani, Kampuni ya Jan International Limited inayojishughulisha na uuzaji magari ilisema asilimia kubwa ya wateja hununua magari ya mwaka 2005, 2006 na 2008 kutokana na bei yake kuwa chini.

Alitolea mfano wa wanunuzi wa magari madogo yaliyotengenezwa mwaka 2010 kushuka chini bei zake huwa ndogo, ambazo huanzia Sh. milioni 15 kulingana na aina ya gari.

Kampuni ya SBT Japan ofisi ya Tanzania, ilisema kwamba mteja anapokwenda kwao na kuchagua gari ya toleo la zamani siyo kwamba analipenda zaidi bali ni kutokana na thamani yake sokoni.

Alitolea mfano mteja anataka kuagiza RAV4 ya mwaka 2012 thamani ya kununua gari hilo nchini Japan ni kubwa na ushuru kwa makisio mteja anatakiwa awe na fedha siyo chini ya milioni 40.

Kwamba RAV 4 toleo la zamani mfano ya 2004 unaweza kutumia Sh. milioni 25 wakati toleo la sasa kuagiza peke yake unaweza kutumia siyo chini ya milioni 20.

Meneja wake alisema siyo kwa watumishi wala wafanyabiashara kwenye asilimia 100 labda wanaoagiza magari ya toleo la sasa ni asilimia tano. Endapo itakuwa hivyo kama walivyoelekeza kwa sababu bado kauli yake haijatolewa ufafanuzi kama yazuiwe kabisa ya chini ya mwaka 2010 au ni mkakati upi utawekwa.

Wauzaji na waagizaji hao wanapendekeza serikali kupunguza kodi, ili kuwezesha wengi kuagiza magari ya kisasa ambayo wanaweza kuyalipia kwa kuwa bei ya kununua huwa ni chini zaidi ya ushuru unaotakiwa kulipwa.

Nipashe tunakubaliana na kuunga mkono jitihada za serikali kuhakikisha nchi yetu haigeuzwi kuwa dampo la bidhaa chakavu, bali tupate mpya, lakini changamoto kubwa ni uwezo wa wananchi wengi kununua kipya na kumudu kodi inayotakiwa.

Watu wengi wanapambana kuwa na magari binafsi kutokana na kwamba usafiri wa umma, bado haujafikia viwango vinavyotakiwa kwa maana ya kwamba mtu anaweza kupanda daladala au hiace akaenda kazini na kurudi kwa urahisi zaidi.

Kama hali ingekuwa hivyo, basi wengi wangeridhika na kuutumia usafiri wa umma katika shughuli zao nyingi, na wengine kutoona ulazima wa kununua magari.

Ili kufikia malengo ni muhimu kuboresha usafiri wa umma, mathalani ujio wa mwendokasi Dar es Salaam walitarajia kila njia yanapopita kutakuwa na ahueni ya usafiri; kwamba mtu ataweza kuegesha gari na kupanda usafiri huo, ili kupunguza magari madogo kuingia katikati ya mji.

Kwa sasa mafuta yamepanda bei kiasi cha wengi kutamani kuegesha magari, lakini wanashindwa kutokana na ubora wa usafiri huo.

Tunatambua jambo hili ni la kisheria, lakini ni muhimu kuangalia hali ya maisha ya watu kwa kuwasaidia wananchi kununua magari kwa ajili ya kuwa na uhakika wa usafiri, na kupunguza uchafuzi wa mazingira kwa kuwa na magari chakavu.

Nia njema ya serikali kuzuia nchi iwe dampo kwa magari, iende hadi kwenye bidhaa nyingine kama za umeme, nguo, viatu na ujenzi ambazo husababisha wananchi kupata hasara, au fedha zao kutumika kwa manunuzi ambayo hayawezeshi maisha yao kubadilika.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com



## Muungwana Lazima Nilonge



# Mwenge wa Uhuru usivumilie miradi ya chini ya kiwango

Na Sabato Kasika

**KATIKA** kuharakisha maendeleo, serikali imekuwa ikitafuta fedha hata za mikopo na nyingine za walipa kodi ili kufikia lengo hilo, kwa kujenga na kuboresha miradi mbalimbali ikiwamo midogo na mikubwa.

Pamoja na juhudi hizo za serikali, kumekuwapo hujuma zinazofanywa kwenye miradi hiyo zinazoweza kusababisha serikali isifikie kile ambacho imekusudia kukifanya kwa ajili ya maendeleo hayo.

Hiyo inajumuisha hujuma kwenye ujenzi wa miradi ya maendeleo chini ya kiwango, hali inayoweza kuiingiza serikali kwenye gharama zisizotarajiwa, kwa kurudia upya ujenzi wa miradi husika.

Kwa mfano, katika mbio za Mwenge wa Uhuru mwaka jana, kiongozi huyo alikataa kuzindua miradi 52 ambayo ilitiliwa shaka kwa kuwa ilikuwa hailingani na thamani ya fedha iliyotumika kuijenga.

Ni hatua iliyoendana na agizo kwa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), kufanya uchunguzi wa miradi hiyo 52 na kuwachukulia hatua mahakamani wote ambao wangebainika katika hujuma hiyo.

Wakati wa kuzinduliwa mbio za Mwenge wa Uhuru kwa mwaka huu wa 2022 mkoani Njombe, kiongozi wa mbio hizo akakumbusha kuwa mbio za Mwenge wa Uhuru zimekuwa ni kichocheo cha maendeleo na kudumisha umoja nchini.

Nikirejea kwenye hujuma katika miradi hiyo, ni kwamba mbio hizo zimekuwa zikiizibua kila mwaka isipokuwa mwaka 2020 ambao hazikufanyika, lakini kumekuwapo matukio ya kukataa uzinduzi wa miradi iliotiliwa shaka.

> **Zaidi anaelekeza viongozi hao kutoa taarifa kwa vyombo vinavyohusika kwa miradi mtakayoitilia shaka ili hatua za kisheria zichukuliwe kwa wale wote watakaobainika kuhusika na hujuma.**

Kwa mfano mwaka 2019, Kiongozi wa Mbio za Mwenge wakati huo, Mzee Mkongea Ally, akagoma kuzindua mradi wa maji uliogharimu zaidi ya Sh. Milioni 200 na wasakwe waliohusika na ubadhirifu wa fedha hizo mradi.

Nadhani kwamba kwa matukio mbalimbali ya hujuma katika miradi ya maendeleo, ingependeza kama safari hii mbio hizo zitaendelea kukwepa miradi ambayo utekelezaji wake uko chini ya kiwango.

Ninaamini kwamba, serikali inapotoa fedha kwa ajili ya maendeleo inatarajia kuona zitatumika ilivyokusudia, kwamba miradi ilingane na thamani ya fedha iliyotumika kwa usimamizi wa watendaji wa maeneo husika.

Hilo ndilo linalomfanya Makamu wa Rais Dk. Philip Mpango awaagize viongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru nchini, kuhakikisha hawazindui miradi watakayoibaini haiendani na thamani ya fedha iliyotumika.

Zaidi anaelekeza viongozi hao kutoa taarifa kwa vyombo vinavyohusika kwa miradi mtakayoitilia shaka ili hatua za kisheria zichukuliwe kwa wale wote watakaobainika kuhusika na hujuma.

Pamoja na hayo, ni vyema watendaji wa serikali wasitumie vyeo vyao kwa manufaa yao, badala yake wasimamie ujezi wa miradi ya maendeleo kwa manufaa ya maeneo wanayoongoza na taifa kwa ujumla.

Vivyo hivyo, wananchi nao kwa upande wao, wawe mstari wa mbele kufuatilia miradi inayotekelezwa kwenye maeneo yao ili waweze kubaini kama utekelezaji wake unalingana na thamani ya fedha iliyotumika.

Njia hiyo inaweza kusaidia kuziba mianya ya hujuma inayotumika kutekeleza miradi chini ya kiwango, hata kuwafanya wenye nia hiyo kuwa waoga kutumia fedha za walipa kodi kwa manufaa yao.

Wananchi wana haki ya kuhoji miradi inayotekelezwa katika maeneo yao, lakini wakikaa kimya, wajanja wachache wataendelea kutumia nafasi hiyo kujinufaisha, badala ya kunufaisha taifa kwa kutekeleza miradi kikamilifu.

Iwapo watajitenga na kudhani hawahusiki kufuatilia miradi kwenye maeneo yao, ni wazi hujuma hizo zinaweza kuendelea kuwapo, hivyo ingefaa wananchi nao wafanye sehemu ya kudhibiti kila aina ya ubadhirifu.

## Utalii wa michoro ya miamba wahimizwa

**Na Peter Haule,** DODOMA

Watanzania wametakiwa kuwa na utamaduni wa kutembelea maeneo yenye hadhi ya urithi wa Dunia ikiwemo michoro ya miamba ya Irangi Kondoa mkoani Dodoma ili kujua historia ya nchi na Serikali inavyohifadhi mali kale kwa manufaa ya kizazi hiki na kijacho.

Rai hiyo imetolewa na Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali Watu wa Wizara ya Fedha na Mipango, Lusius Mwenda, wakati wa ziara ya utalii wa ndani wa watumishi 40 wa Ofisi ya Rais Fedha na Mipango, Zanzibar katika michoro ya miambani Irangi Kondoa mkoani Dodoma.

Mwenda alisema lengo la ziara hiyo ni watumishi waliotoka Zanzibar pamoja na mambo mengine ni kujua fursa za utalii zilizopo Tanzania Bara na kuwa mabalozi kwa wengine wa mali kale adimu nchini.

Muhifadhi na Mkuu wa Kituo cha Michoro ya Kondoa Irangi, Zuberi Mabie, alisema michoro ya miambani iliyopo Irangi Kondoa ni miongoni mwa hifadhi za mali kale zilizoingizwa katika hadhi ya urithi wa Dunia mwaka 2006 chini ya Shirika la Kimataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO).

Alisema maeneo hayo ya mali kale yana manufaa makubwa kiuchumi kwa kuwa yanatoa fursa ya ukusanyaji wa mapato ya Serikali ambayo mapato hayo yanaenda pia kufanya shughuli mbalimbali za maendeleo ya wananchi.

Mabie aliwapongeza watumishi hao kutoka Zanzibar kwa kuona umuhimu wa kutembelea michoro hiyo na kujionea jitihada za Serikali za kuihifadhi na kuwataka watumishi kuwa sehemu ya kuhifadhi maeneo hayo muhimu.

Mtumishi wa Ofisi ya Rais Fedha na Mipango Zanzibar, Saada Said Seif, alishukuru kwa kupata fursa ya kuona michoro hiyo ambayo alikiri imemvutia na kuwaomba wananchi wengine hususani kutoka Zanzibar wafanye utalii wa ndani wa kwenda kuangalia michoro hiyo.

Michoro ya miambani Kondoa yenye rangi nyeupe, nyekundu na nyeusi inasadikiwa kuchorwa na wawindaji na waokota matunda hasa wa kabila la Wasandawe miaka 1,500 mpaka 50,000 iliyopita, huku michoro ya rangi nyekundu ikidhaniwa kuwa ya muda mrefu zaidi.

Maeneo mengine yaliyoingizwa kwenye urithi wa Dunia chini ya UNESCO ni Mji Mkongwe wa Zanzibar, Fifadhi ya Taifa ya Serengeti, hifadhi ya mlima Kilimanjaro, magofu ya Kilwa na Songo mnara na Pori la Akiba la Selous.

# Mbaroni tuhuma utoroshaji dhahabu

**Na Happy Severine,** BARIADI

WATU watatu wamekamatwa kwa tuhuma za utoroshaji wa dhahabu katika Wilaya ya Bariadi mkoa wa Simiyu yenye uzito wa gramu 10.

Kutokana na kitendo hicho, Mkuu wa mkoa huo, David Kafulila, aliwitaka vyombo vya ulinzi na usalama kuimarisha ulinzi maeneo ya migodi.

Kafulila ameitaka Idara ya Madini kwa kushirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama kuimarisha ulinzi na kufanya ukaguzi maalumu kwenye migodi yote mkoani humo kwa kuwakamata wote wanaojihusisha na utoroshaji wa madini.

Alitoa maagizo hayo jana alipokuwa akizungumza na maofisa wa Jeshi la Polisi na waandishi wa habari katika kituo cha Polisi Bariadi baada ya kuwahoji watuhumiwa waliotorosha madini katika mgodi wa Dutwa uliopo Bariadi.

"Najua nyie mmetangulizwa, nawatafuta walioko nyuma yenu, mkiwataja mtapata nafuu na msipowataja mtakuwa kafara...watajeni watu wanaowatuma katika mambo hayo, RPC hakikisheni mnafanya ukaguzi maalumu na naamini vyombo mnajua jinsi ya kufanya," alisema Kafulila na kuongeza:

"Hawa ambao wamekamatwa tunataka waione rangi ya Rais Samia, kamateni wote kwa sababu hatuwezi kuruhusu hiyo mianya kuwapo, vikosi kazi vilivyoundwa na watu wa usalama hakikisheni mnazibadilisha."

Ofisa Madini Mkoa wa Simiyu, Mhandisi Amini Msuya, alisema walikamata gramu 10.4 mbichi, baada ya kuchomwa zilibaki gramu saba ambazo zilikuwa hazieleweki zinakoelekea, na kwamba watu hao walikamatwa kwa taarifa za kusafirisha dhahabu hiyo kwenda Kenya.

Alisema wanashirikiana na vyombo vya usalama kuhakikisha wanafanya uchunguzi kwa watu hao ili kupata mtandao wa utoroshaji wa dhahabu kwa lengo la kuuvunja na pia wanatoa elimu kwa wafanyabiashara waweze kufuata taratibu za biashara ya madini.

Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Simiyu, Kamishna Msaidizi wa Polisi, Shadrack Majisa, alisema jeshi lake liko tayari kushirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama ili kudhibiti utoroshaji wa madini, na kwamba wataendelea kuimarisha ulinzi katika maeneo ya migodi.

Yunis Masuke (mtuhumiwa wa utoroshaji wa dhahabu) alisema yeye ni msimamizi wa mwalo na kwamba alikamatwa kwa tuhuma za kuuza dhahabu gramu 10.4 kwa Prisca Seni ambaye naye pia ameshakamatwa.

Gamaya Makoye, mlinzi wa mgodi wa EMJ, alisema alikamatwa baada ya Yunisi Masuke na Prisca Seni kuziana dhahabu, huku yeye akiwa ni mlinzi wa eneo hilo.




Makamu Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Tanzania Bara, Abdulrahman Kinana, akipiga kura ya kumchagua Mwenyekiti wa Shina Namba 9 Tawi la Masaki, Kata ya Msasani, Wilaya ya Kinondoni, mkoani Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mwenyekiti kortini madai ya rushwa

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

MWENYEKITI wa Kijiji cha Nyakabale, Kiraryo Nzagamba (45), amefikishwa katika Mahakama ya Wilaya ya Geita kwa tuhuma za kuomba na kupokea rushwa ya Sh. 300,000.

Nzagamba anadaiwa kupokea fedha hizo kutoka kwa Amos Said ili aendelee kubakiza jina lake kwenye mkataba wa ulinzi kati ya kijiji hicho na kampuni ya uchimbaji madini ya Geita Gold (GGML) kitendo ambacho ni kinyume cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa.

Mshtakiwa huyo alipandishwa kizimbani jana mbele ya Hakimu Mkazi Mfawidhi, Samuel Maweda, na aliposomewa shtaka lake alikana na yuko nje kwa dhamana.

Upande wa mashtaka ukiongozwa na Wakili Kiongozi wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Geita, Kelvin Murusuri, ulidai kuwa upelelezi wa kesi hiyo umekamilika na kuomba mahakama iridhie kumsomea mshtakiwa maelezo ya awali.

Hakimu Maweda alikubaliana na ombi hilo na kumuuliza mshtakiwa kama yuko tayari kusomewa maelezo ya awali na kujibu ndiyo.

Akisoma maelezo ya awali, Murusuri alidai kuwa kati ya Januari na Juni, 2021 katika wilaya ya Geita, mshtakiwa katika kutekeleza majukumu yake akiwa Mwenyekiti wa Kijiji cha Nyakabale, aliomba hongo ya Sh 300,000 kutoka kwa Said ili aendelee na mkataba wa ulinzi katika mgodi wa GGML.

Baada ya kusomewa mashtaka, mshtakiwa alikubali kwamba kijiji cha Nyakabale kina makubaliano ya kimkataba ya uhusiano wa ulinzi na GGML na kwamba kwa mujibu wa makubaliano hayo, kijiji kina jukumu la kuchagua vijana kutoka katika kijiji hicho kwa lengo la kufanya kazi ya ulinzi katika mgodi.

Pia mshtakiwa alikubali kwamba wao ndiyo wana jukumu la kuwalipa vijana wanaofanya kazi ya ulinzi GGML baada ya GGML kulipa fedha katika kijiji hicho.

Murusuri alimhoji mshtakiwa kuhusiana na kupokea hongo ya Sh 300,000 kutoka kwa Said na kukana.

Baada ya Wakili Murusuri kumaliza kumsomea mshtakiwa huyo maelezo ya awali, alidai kuwa upande wa Jamhuri unatarajia kupeleka mahakamani mashahidi wanne na vielelezo vinne kisha kuomba mahakama kupanga tarehe ya kuanza kusikiliza mashahidi wa upange wa Jamhuri.

Hakimu alikubaliana na ombi hilo na kuahirisha kesi hiyo hadi Mei 18, mwaka huu, kwa ajili ya kuanza kusikiliza mashahidi wa upande wa Jamhuri.

# China kuonyesha tukio la kuhama nyumbu Serengeti

**Na Faustine Feliciane**

KITUO cha Utamaduni cha China nchini kimepanga kuonyesha na kurekodi tukio la aina yake la kuhama kwa nyumbu kutoka Hifadhi ya Taifa ya Serengeti kwenda Maasai Mara nchini Kenya.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na kituo hicho juzi, mpigapicha maarufu wa wanyamapori, raia wa China, Chen Jianxing, amesafiri kutoka China kwa ajili ya kushuhudia tukio hilo pamoja na kupiga picha.

Tukio hilo la kuhama kwa nyumbu linawakusanya wapiga picha mbalimbali pamoja na watalii kutoka sehemu mbalimbali kushuhudia tukio hilo.

Akizungumzia tukio hilo Mkurugenzi wa Kituo hicho, Wang Siping, alisema kituo hicho kupitia mitandao yake itaonyesha tukio hilo ikiwa ni sehemu ya kutangaza utalii wa Tanzania.

"Tanzania inajulikana kuwa paradiso ya wanyamapori mara nyingi inaitwa 'bustani ya Edeni ya wanyamapori'. Tangu miaka ya 1950, hifadhi za taifa 22 na msururu wa hifadhi za asili zimeanzishwa na serikali ya Tanzania ili kulinda viumbehai. Hifadhi kama Serengeti, Ngorongoro, na Kilimanjaro ambazo jumla ya takriban moja ya tatu ya ardhi yake imetengwa kulindwa. Kati yao, maeneo saba yameteuliwa kama maeneo ya Urithi wa Dunia na UNESCO (Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni)," alisema.

Pia Wang alisema kwa miaka mingi Tanzania na Kenya zimekuwa marafiki na kusaidia katika maeneo mbalimbali ya kimaendeleo.

"Miaka 58 iliyopita imeshuhudia urafiki mkubwa kati ya China na Tanzania. Maelfu ya raia wa China wamekuja katika nchi hii nzuri kufanya kazi au kusafiri na wengi wao wamekaa hapa kwa miongo kadhaa, wakiona Tanzania kuwa mji wao wa pili na kuchangia mawasiliano kati ya nchi hizo mbili, miundombinu, maendeleo ya kiuchumi, huduma ya afya ya Tanzania, na kubadilishana watu kwa watu kati ya nchi mbili.

"Tunatumai kwa dhati Wachina wengi zaidi watamfuata Chen Jianxing na kuunga mkono kikamilifu utafiti na ulinzi wa wanyamapori nchini Tanzania na kupata mafanikio makubwa katika mabadilishano ya watu kati ya China na Tanzania," alisema Wang.

Alisema wachina wengi wataendelea kuja Tanzania kutalii na kufanya shughuli nyingine za kimaendeleo.

Mkurugenzi wa Jumuiya ya Uhifadhi wa Wanyamapori (WCS), Tim Davenport, alisema tukio hilo ni la aina yake na linapaswa kutangazwa kutokana na juhudi za Tanzania katika kulinda wanyamapori na maz-




Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, akizungumza wakati wa uzinduzi wa Studio mpya ya TBC 2, mkoani Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# DAWASA yapeleka maji shule inayolea yatima

**Na Joseph Mwendapole**

MAMLAKA ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA), imepeleka huduma ya maji safi kwenye shule ya Watoto Wetu Tanzania, iliyoko Chalinze mkoani Pwani.

Shule hiyo inayohudumia watoto yatima na wanaoishi katika mazingira magumu, imekuwa na shida ya maji kwa muda mrefu, hivyo kulazimika kutumia maji ya visima yanayopatikana mbali.

Akizungumza na gazeti hili jana, msimamizi wa mradi huo, Prosper Nyagawa, alisema mamlaka hiyo imeamua kuwapelekea maji baada ya kuona changamoto ya kukosa huduma hiyo kwa muda mrefu.

Alisema kazi iliyofanyika ni kutoa maji kwenye Kijiji cha Mazizi kilichopo kata ya Mazizi kwa kutumia bomba la inchi tatu na kupeleka maji kwa umbali wa kilomita 5.5.

"Kazi imekamilika na sasa wanafunzi wameanza kupata huduma ya majisafi sisi tunajua kwamba huduma ya maji ni muhimu kwa kila mtu, hivyo tumeona kuna haja kwa kituo hiki cha watoto kupata majisafi ili waweze kukidhi mahitaji yao muhimu ya kila siku," alisema.

Naye mwasisi wa shule hiyo, Evance Tegete, aliishukuru DAWASA kwa kufikisha huduma ya majisafi kwenye shule yao.

"Tulikuwa na shida kubwa ya majisafi kwenye shule yetu na kwa muda mrefu tumekuwa tukinunua maji ya visima maeneo ya mbali na kwa gharama kubwa," alisema Tegete.

"Hali ya ukosefu wa maji ilitupa wakati mgumu hasa kutokana na idadi kubwa ya watoto wanaoletwa shuleni hapa lakini kwa sasa tumepata ahueni kubwa tunawashukuru sana kwani huduma hii kwetu tunaona kama ni ndoto kwetu," alisema

Shule ya Watoto Wetu Tanzania ilianzishwa mwaka 2013 na inahudumia watoto yatima 69.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Mazizi, Ramadhan Rajabu alisema huduma ya maji kwenye shule hiyo imekuwa msaada mkubwa kwani wananchi wa maeneo hayo wamekuwa wakipata shida ya kutafuta majisafi maeneo ya mbali.

Alisema shule hiyo imekuwa ikitoa msaada mkubwa kwa watoto wasio na walezi na wale wanaoishi katika mazingira magumu kwenye kijiji cha Mazizi. "Nawapongeza DAWASA kwa maboresho makubwa ya huduma ya maji yanayofanywa kwenye maeneo mbalimbali ya mji wa Chalinze na kutufikishia huduma hii hapa mmefanya jambo la maana sana," alisema.

## DC aonya wachochezi uthamini Bwawa Mindu

**Na Idda Mushi,** MOROGORO

WANASIASA wametakiwa kuacha uchochezi kwa wananchi dhidi ya Serikali kwenye tathmini na uthamini unaoendelea kwenye Bwawa la Mindu mkoani Morogoro.

Tathmini na uthamini ni sehemu ya utekelezaji wa maazimio ya mawaziri wa wizara nane za kisekta kuhusu mgogoro wa ardhi na mipaka katika maeneo mbalimbali nchini.

Mkuu wa Wilaya ya Morogoro, Albert Msando, alitoa angalizo hilo wakati akizungumzia tathmini na uthamini wa hifadhi ya mita 500 katika bwawa la Mindu linaloendelea kufanyika na kubainisha mwaka 2022 Rais Samia Suluhu Hassan kwa kujali wananchi aliagiza kufanyika upya tathmini na uthamini huo.

"Mhe Rais alitaka kujua idadi kamili ya wananchi waliopo ndani ya mita mia tano,ionyeshwe athari za uwepo wao na gharama za kuwaondoa endapo itabidi, na katika hali ya kawaida lazima kama wilaya tutambue mita hizo na walipofikia wataalamu , Mtaa wa Kasanga wameshafanyiwa tathmini, hakuna mahali ambapo zoezi la kubomoa nyumba ama kuondolewa kwa nguvu," alisema na kuongeza:

"Limefanyika, na zaidi hatuwezi kushauri wala kuchukua uamuzi wowote bila tathmini na uthamini."

Aliwaonya baadhi ya viongozi wa kisiasa kuacha kukwamisha zoezi hilo na kwamba yeyote anayemshawishi mwananchi kupinga atachukuliwa hatua kwa kuwa zoezi hilo sio la mtu binafsi bali kwa mujibu wa sheria.

Alimtaka Diwani wa Mindu kujiridhisha na matakwa ya kisheria kama kweli ana nia ya dhati kuwatetea wananchi kwani sheria ya maji namba 221 ya mwaka 2016 iko wazi kuhusu suala hilo na kwamba mgogoro wa Mindu ulianza tangu mwaka 2002 na kushughulikiwa kwa nyakati tofauti.

Msando alibainisha kuwa usimamizi wa bwawa la Mindu upo chini ya Bonde la Wami Ruvu ambao walikabidhiwa na baraza la madiwani la Manispaa ya Morogoro, wakazi wa kata hiyo walieleza hofu yao juu ya zoezi la tathmini na uthamini kwenye upimaji wa mita 500 katika bwawa la Mindu huku wakiomba kuundwa kwa tume huru wakati wa zoezi hilo la upimaji.

Mwenyekiti wa mtaa wa Mindu Shomari Athumani alisema wanaamini kinachoendelea ni kinyume na makubaliano kutokana na vipimo wanavyopimia kutoonyesha uhalisia na kuomba Rais Samia kuingilia kati kuwasaidia.

## Kongamano kujadili vikwazo vya elimu Tabora

**Na Mwandishi wetu**

MAADHIMISHO ya Juma la Elimu (GAWE) yanatarajiwa kufanyika Igunga mkoani Tabora kuanzia Aprili 25 hadi 29 mwaka huu.

Kwa mujibu wa waandaaji wa maadhimisho hayo ambao ni Mtandao wa Kitaifa wa Mashirika yasiyo ya kiserikali yanayojishughulisha na elimu nchini (TEN/MET), yataongozwa na kaulimbiu inayosema 'tuwekeze katika elimu, kwa elimu bora na ujumbe wa elimu kwanza'.

Kwa Mujibu wa Kaimu Meneja Programu wa TEN/MET, Alistidia Kamugisha, kutakuwa na shughuli mbalimbali zitakazoambatana na maadhimisho ya juma hilo ikiwamo kongamano la elimu ambalo litaangazia kwa mapana changamoto za elimu katika mkoa wa Tabora.

"Mkoa wa Tabora umechaguliwa kufanyiwa maadhimisho ya juma la elimu kwa lengo la kuungana na wenyeji kwa ajili ya kuongeza nguvu katika kuhamasisha upatikanaji wa elimu bora kwa watoto wote,"alisema Kamugisha.

"Tunatambua juhudi mbalimbali zinazoendelea katika mkoa huo kwa lengo la kufanikisha upatikanaji wa elimu bora kwa wote, lakini si vibaya pia na TEN/MET kama mtandao wa elimu wa kitaifa kushirikiana pamoja nao ili kuongeza nguvu zaidi na kufikia malengo."

Kamugisha alisema kuendelea kufanyika maadhimisho hayo ya juma la elimu katika mikoa tofauti kila mwaka kumesaidia kwa kiwango kikubwa kuchechemua maendeleo ya elimu kwenye mikoa na wilaya husika.

"Kwa mfano kwa mwaka juzi yalifanyika wilaya ya Chemba mkoa wa Dodoma na mwaka jana yalifanyika mkoani Mara wilaya ya Rorya na yamesababisha mabadiliko makubwa sana ikiwamo kuongeza mwamko wa jamii zilizotembelewa katika ushiriki wa masuala ya elimu na kuondokana na mila potofu," alisema Kamugisha.

"Lakini pia katika wilaya ya Chemba, wadau walichangia umaliziaji bweni la wasichana la Kwamtoro na michango mbalimbali ambayo ilisaidia kuongezea nguvu ya ujenzi wa vyumba vya madarasa katika shule za msingi zilizotembelewa. Kwa upande wa Rorya wadau wa juma la elimu walichangia na kununua vifaa vya ujenzi, na wadau hao hao pia walichangia ununuzi wa madawati na viti kwa ajili ya maabara ya Shule ya Sekondari Bukama."

Alisema kwa mwaka huu wanatarajia kwamba miongoni mwa vitu ambavyo juma hilo la elimu litasaidia ni umaliziaji wa bweni la wanafunzi wenye mahitaji maalum wa shule ya msingi Igunga.

"Shule ya Msingi Igunga ni moja kati ya shule jumuishi nchini zinazopokea wanafunzi wenye ulemavu. Shule hii ina wanafunzi 1,245 kuanzia darasa la kwanza hadi la saba na kati yao wanafunzi 35 wana ulemavu wa uono hafifu, mtindio wa ubongo, viziwi na ulemavu wa viungo, kwa hiyo, ukamilishaji wa ujenzi wa bweni hili utakwenda kuwasaidia watoto wenye ulemavu wa kike 80 ambao watakuwa wanaishi humo."

Mwakilishi wa wadau wa elimu wa taasisi ya Shule Direct, Denish Otieno, alisema sekta ya elimu ni muhimu kwa maendeleo ya nchi, hivyo wao watahakikisha wanaendelea kushirikiana na serikali na wadau mbalimbali katika kuendeleza sekta hiyo.

# Mwenge washtukia ufisadi ujenzi vyumba vya madarasa

**Na Hamisi Nasri,** MASASI

KIONGOZI wa mbio za Mwenge wa Uhuru kitaifa, Sahili Nyangabala Nyeraruma, amekataa kuzindua mradi wa ujenzi wa vyumba vitatu vya madarasa viliyvojengwa katika Shule ya Msingi Mkuti Halmashauri ya Mji Masasi mkoani Mtwara yaliyojengwa gharama ya shilingi milioni 52.6 kutokana na kujengwa chini ya kiwango.

Mradi huo ambao umetekelezwa na serikali kuu, halmashauri pamoja na nguvu za wananchi, baada ya kiongozi huyo kuukagua alibaini kuwapo kwa kasoro kadhaa ambazo zilimfanya kukataa kuuzindua.

Kiongozi huyo alisema amekagua mradi huo kwa kina na hajaridhishwa na hali ya ujenzi, na kwamba baada ya kufanya ukaguzi wake amebaini kuwa mradi huo una kasoro, hivyo haustahili kuzinduliwa wakati wa mbio za Mwenge.

"Siwezi kuzindua mradi huu wa vyumba vitatu vya madarasa hapa kwa sababu sijarishwa kabisa na ujenzi huu, umejengwa chini ya kiwango na fedha zimetumika vibaya, naagiza Takukuru kuchunguza mara moja ujenzi huu," alisema,

Alisema kuwa madarasa hayo yamejengwa chini ya kiwango au ubora unatakiwa kama serikali inavyotaka na kwamba hata ukiangalia kwa haraka haraka kasoro zilizopo zinajionesha wazi.

Nyeraruma alieleza kwamba baadhi ya kasoro ambazo zipo katika ujenzi huo ni uwekaji wa madirisha pamoja na sakafu ambayo imewekwa kwa kutumia vigae visivyo na ubora. Alisema hivyo kwa ujumla katika mradi fedha zimetumika vibaya na mradi kukosa thamani ya fedha halisi licha ya wananchi pia kutumia nguvu zao katika kuufanikisha.

Awali akisoma taarifa ya mradi , mhandisi wa Halmashauri ya Mji wa Masasi, Ombeni Usiri, alisema jumla ya gharama ya mradi huo ni Sh. 52.667,250 ambapo Sh. 5,000,00 zilitolewa na Rais, michango ya wahisani ikiwa ni Sh. 6.619,500, michango ya wananchi Sh. 3,809,250 huku halmashauri ikichangia Sh.37,238,500/.

Usiri alisema halmashauri itazifanyia kazi changamoto zote zilizojitokeza katika mradi huo na kueleza kuwa kasoro hizo ni za kawaida, na kwamba wamepokea maagizo hayo.

Akipokea Mwenge ukitokea Wilaya ya Nanyumbu, Mkuu wa Wilaya ya Masasi, Claudia Kitta, alisema katika wilaya jumla ya miradi 11 itazinduliwa na kuwekwa mawe ya msingi katika halmashauri ya Mji Masasi na Halmashauri ya Wilaya ya Masasi.



Baadhi ya waumini wa dini ya kiislamu, wakiwa katika foleni ya kupata futari iliyoandaliwa na Taasisi ya Whoishussain ya Arusha, katika Kata ya Olorieni, jijini humo juzi, ambapo zaidi ya waumini 500 walishiriki. **PICHA: TUMAINI MAFIE**

# Ajeruhiwa akitoka kibandaumiza usiku

**Na Idda Mushi,** MLIMBA

MKAZI wa Kijiji cha Ipugasa Kata ya Utengule Tarafa ya Mlimba katika Halmashauri ya Wilaya ya Mlimba mkoani Morogoro, Said Hussein Matola, amevamiwa na kupigwa hadi kujeruhiwa ikiwamo kuvunjwa mikono na miguu.

Alipatwa na madhila hayo wakati akirejea nyumbani kutoka kuangalia pambano la soka kati ya Simba na Orlando Pirates majira ya usiku.

Akizungumza na Nipashe katika Kituo cha Afya Mlimba alipolazwa,Matola alidai kuvamiwa na watu ambao baadhi anawafahamu akiwamo kiongozi mmoja wa Kijiji, na kumpiga katika maeneo mbalimbali ya mwili wake ikiwamo mikononi, miguuni, kichwani na puani kwa kutumia fimbo za jadi maarufu kama milanga.

Matola anasema: "Nikiwa njiani kutokea kwenye kibanda umiza kwenda nyumbani ,ghafla nikavamiwa na watu wanne waliotokea kwenye shamba la mahindi na kuanza kunipiga kwa fimbo...nilipiga kelele za kuomba msaada na walipoona watu wanasogea eneo la tukio, wakakimbia."

Akadai anaamini chanzo cha tukio hilo ni kitendo chake cha kuhoji mara kwa mara matumizi ya fedha za maendeleo ya kijiji na miradi ambayo wanadhani yametumiwa vibaya na kila anayehoji kuonekana adui.

"Watu wengi wanaohoji taarifa za mapato na matumizi huonekana maadui, na wengine wameshajikuta wakitengenezewa kesi au kupitia madhila mbalimbali," aliongeza.

Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Ipugasa, Charity Kisepe, alikiri kutokea kwa tukio hilo na kukanusha tuhuma kuwa mmoja wa viongozi wa kijiji hicho kuhusika, na kwamba tukio hilo linahusishwa na wivu wa kimapenzi.

Watu wawili wanadaiwa kushikiliwa kituo cha Polisi Mlimba wakituhumiwa kuhusika na tukio hilo.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro, Fortunatus Muslimu, hakupatikana jana kuzungumzia tukio hilo.

# Spika atoa ushauri kuhusu ujenzi wa barabara

SPIKA wa Bunge, Dk.Tulia Ackson, ameshauri serikali kuweka utaratibu wa kuzitengea fedha za matengenezo madogo barabara ambazo zimejengwa kwa kiwango cha lami ili kuondokana na gharama za kuzijenga upya.

Dk. Tulia alitoa ushauri huo jana bungeni baada ya Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Godfrey Kasekenya, kujibu swali la nyongeza la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Aleksia Kamguna.

Katika swali lake, Mbunge huyo alisema serikali imekuwa ikitumia fedha nyingi kujenga barabara lakini kwa muda mfupi huwa zinaharibika na kuota nyasi.

"Serikali ina mpango gani wa kutenga fedha za matengenezo ya barabara hizi ili kuzinusuru?" alihoji.

Akijibu swali hilo, Kasekenya alisema barabara nyingi za changarawe na vumbi hazidumu kwa muda mrefu na hutengewa fedha kwa ajili ya matengenezo kila mwaka na kwamba azma ya serikali ni kujenga barabara zote kwa kiwango cha lami.

Alisema ujenzi wa barabara hizo ni gharama na zinategemea upatikanaji wa fedha.

"Barabara kubwa za kimkakati ndizo zitakazoanza kujengwa kwa lami kadri upatikanaji wa fedha utakavyoruhusu," alisema.

Kutokana na majibu hayo, Spika Tulia alisema fedha nyingi zimekuwa zikitumika kujenga barabara hizo lakini matengenezo huwa hayafanyiki, hivyo kusababisha kuharibika kwa kiwango kikubwa hatua ambayo hulazimisha kuondoa lami na kujenga upya.

"Kinaanza kishimo kidogo kinaachwa hadi linakuwa kubwa. Matokeo yake tunarudi kule nyuma fedha zinatumika nyingi sana kutengeneza upya hizo barabara. Barabara ya kutoka hapa kwenda Iringa hilo ni janga hiyo ni ya kuondoa yote si ya mashimo, lakini barabara ya Mbeya Mjini kwenda Chunya ile barabara imejengwa kwa fedha nyingi sana na kwa sasa ina mashimo.

"Matokeo yake magari yatakuwa yanapitiliza tu bondeni hoja ya Mbunge mnapotenga fedha za kujenga barabara ya changarawe zitengwe na za matengenezo, na mnapotengeneza za lami mtenge na za matengenezo ili ikionekana dosari ndogo ishughulikiwe mapema kabla haijawa tatizo kubwa," alisema.

Katika swali la msingi, Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Mwanaisha Ulenge, alihoji ni upi mkakati wa serikali wa kuunganisha barabara za mkoa wa Tanga na mikoa jirani. Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Kasekenya alisema mpango wa serikali ni kuiunganisha mikoa yote kwa barabara za lami.

"Mkoa wa Tanga unapakana na mikoa ya Pwani, Morogoro, Manyara, Kilimanjaro na nchi jirani ya Kenya. Tanga imeunganishwa na barabara zifuatazo Tanga - Chalinze (Pwani), Handeni - Turiani - Magole (Morogoro), Handeni - Kibirashi - Kibaya (Manyara), Tanga - Korogwe - Same (Kilimanjaro), Tanga - Horohoro (Kenya),"alisema.

Hata hivyo, alisema ziko barabara zingine ambazo zinaunganisha mkoa wa Tanga na mikoa jirani.



Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, akiongoza mkutano wa saba wa Bunge kikao cha nane, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Nyumba 300 watumishi afya kujengwa

WIZARA ya Afya imesema katika mwaka wa fedha wa 2022/23 itajenga nyumba 300 za kukaa familia tatu kwa kila nyumba.

Naibu Waziri wa Afya, Dk. Godwin Mollel, aliyasema hayo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Nora Mzeru.

Katika swali lake, Mzeru alihoji serikali ina mpango gani wa kuwajengea wahudumu wa kada mbalimbali za afya nyumba bora ili kuboresha makazi yao.

Akijibu swali hilo, Dk. Mollel alisema katika mwaka wa fedha wa 2021/22, serikali imejenga nyumba 176 na katika mwaka wa fedha 2022/23 itajenga nyumba 300 za kukaa familia tatu kwa kila nyumba.

Katika swali la nyongeza, Mbunge wa Nyang'wale (CCM), Hussein Amar, alisema katika wilaya ya Nyang'wale kumekuwa na mwamko mkubwa wa vijana kuendesha pikipiki na wamekuwa wakipata ajali huku Hospitali ya Wilaya ikiwa haina mashine ya X-Ray.

"Serikali ina mpango gani wa kutununulia X-Ray katika hospitali ya wilaya?" alihoji.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Mollel alisema mkakati wa serikali ni kuhakikisha ajali zinapungua na kwamba suala la upatikanaji wa mashine hiyo waonane na Mbunge ili kuangalia namna ya kupatikana mashine hiyo.

# Uzalishaji mhogo wafikia tani 860

BUNGE limeelezwa kuwa kupitia mradi wa kufufua zao la mhogo katika mkoa wa Mtwara, uzalishaji umeongezeka kutoka tani 611,210 mwaka 2016/17 hadi tani 866,676, mwaka 2019/20.

Naibu Waziri wa Kilimo, Anthony Mavunde, alibainisha hayo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum, Tunza Malapo.

Katika swali lake, mbunge huyo alihoji serikali ina mkakati gani wa kufufua kilimo cha mhogo katika mkoa wa Mtwara.

Akijibu swali hilo, Mavunde alisema uzalishaji huo umeongezeka kutokana na kuongeza utoaji wa huduma za ugani na uzalishaji wa mbegu bora za zao hilo.

Awali, Mavunde alisema serikali kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo, ilianzisha mradi wa kufufua zao la mhogo katika Kanda ya Ziwa na Kanda ya Pwani, ukiwamo mkoa wa Mtwara mwaka 2015.

"Awamu ya kwanza ya mradi huo iliisha mwanzoni mwa mwaka 2021 na awamu ya pili ilianza Desemba, 2021 na inategemewa kuisha mwaka 2024. Kupitia mradi huu uzalishaji wa mhogo katika mkoa wa Mtwara umeongezeka kutoka tani 611,210 mwaka 2016/2017 hadi tani 866,676 mwaka 2019/2020 kutokana na kuongeza utoaji wa huduma za ugani na uzalishaji wa mbegu za mhogo," alisema.

Pia alisema vipando bora vya mhogo vimeongezeka kutoka pingili milioni 30.5 mwaka 2019/20 hadi pingili milioni 40.96 mwaka 2020/21 zenye uwezo wa kutoa mavuno mengi, kuhimili mabadiliko ya tabianchi na magonjwa zilizalishwa na kusambazwa kwa wakulima.






Ukurasa 12

## Ripoti LHRC: Jinsia ina ahueni, ila kuna mengi bado ni shida



Ukurasa 13

Zimejaa utatanishi wa kinachotawala kikuu ama ni sera au ukabila?



Ukurasa 14

## Rais Mobutu wa Zaire na safari alikotoka, kutumika hadi kuishia

siasa

JUMATANO APRILI 20, 2022

Nipashe

HABARI BORA NA KAMILIFU

KADA MGANA MSINDAI

# Aibuka na kuanika kilichompata safari ya Chadema, kurejea CCM

• Afunguka sinema ya kumfuata Lowassa • Alipoenda 'moto' na aliporudi vijembe • Leo; ampigia makofi, amshauri Samia

**Na Richard Makore,** MWANZA

LINAPOTAJWA jina la Mgana Msindai katika medani za siasa nchini siyo geni masikio mwa watu wengi, hasa wenye utashi mkubwa wa siasa za nyumbani lazima wahoji 'yuko wapi huyu?'.

Kwa muonekano 'hajambo' na ana mwili hasa, huku katika siasa zama zake ametikisa kweli, hata akaacha nyayo za kihistoria ndani ya kambi zinazochuana kisiasa, bungeni akiwa na mbwembwe za namna yake, wakati fulani akajibatiza jina la taasisi mojawapo maarufu ya fedha nchini.

Ghafla ndani ya miaka kadhaa ikiwa imeshapita, amekuwa kimya hata wengi hawajui alikotokomea. Hapo ndio juhudi za Nipashe ikasaka nyayo zake ziliko na kumuibua, wengi hawakujua anafanya nini ndani ya kimya kikuu.

Kama kawaida yake, akiwa mtulivu anafuatilia kwa karibu siasa zinazoendelea nchini, ameibuka na salamu zake kuhusu akionacho na kinachoendelea katika siasa nchini

Ndani ya siasa hizo, pia Msindai ambaye mara nyingi amesikika kwa mbwembwe kisiasa bungeni kati ya mwaka 2000 na 2010 na nje ya bunge, hadi wakati fulani akijibatiza jina 'CRDB' ambayo ni benki kubwa nchini.

Kwanini hivyo? Nipashe ilimdadisi kutaka kupata undani wake na hapo ndipo mwenyewe akafafanua kuwa chombo hicho kina historia ya kumsaidia sana kiuchumi, huku binafsi akisifu ufanisi wake uliomvutia, hata naye akajibatiza jina hilo, ili naye abebe umaarufu tajwa.



Mgana Msindai, katika maisha mapya ndani ya Chadema, akiwa na Mwenyekiti, Freeman Mbowe. **PICHA: MTANDAO**

**ALIVYOGEUKA KICHAMA**

Kuna wakati Msindai akiwa kada mwandamizi wa CCM, alionyesha mabadiliko makubwa mwaka 2015 pale kulipotokea mvutano ndani ya chama hicho tawala kupata mgombea urais, yeye akiwa katika kundi linalomuunga mkono, Edward Lowassa, kuwa mgombea wa chama hicho.

Anaiambia Nipashe kuwa binafsi ulikuwa wakati mgumu kwake kufika hatua kuihama CCM na kujiunga na kumfuata CHADEMA wakiwa na wenzake wengine, kutoka CCM, wakimfuata Lowassa alikohamia, kwa ahadi kuwa mgombea urais, baada ya kuenguliwa mapema ndani ya CCM .

Kwa mara ya kwanza Msindai anakiri hadharani kwa undani kwamba kilichomvuta yeye na makada wengine wa CCM kwenda CHADEMA, ni mapenzi yao kwa aliyekuwa Waziri Mkuu, Edward Lowassa aliyehamia huko, akiwa na ufafanuzi wa anachokidai kuwa 'dhamira njema ya Lowassa kwa nchi.'

Anasema hicho kilimsukuma kuihama CCM, kumfuata anakoenda Chadema, akiamini kulikuwa sehemu sahihi katika safari hiyo waliyoiita 'ya matumaini' wakiwa na imani kubwa, Lowassa angeibuka rais kwenye uchaguzi wa mwaka 2015, dhidi ya mpinzani wake Dk. Magufuli wa CCM.

Akisimulia mkasa huo kutoka nyumbani kwake, Pasiansi jijini hapa, anasema kabla ya Lowassa kuondoka CCM baada ya jina lake kukatwa kwenye vikao vya awali, kulikuwapo sintofamu kubwa ndani ya chama hicho kikongwe nchini, akisema hata yeye baada ya kupata taarifa akiwa na baadhi ya makada wa CCM wanaomuunga mkono Lowasa, hawakukubaliana na uamuzi huo.

Haukupita muda mrefu, yeye akiwa na makada wenzake wakiwamo wenye vyeo kama vyake, wenyeviti wa CCM wa mikoa, walihama kuungana na Lowassa, kujiunga na Chadema ambako alinuia kuwania nafasi hiyo ya urais.

Lowassa aliungwa mkono katika uchaguzi huo pia na vyama vinne vya upinzani vya NLD, NCCR- Mageuzi, CUF, yeye Msindai akiwania kiti cha ubunge wake wa zamani, kwa kofia ya Chadema. Hata hivyo, hakupita.

Anasimulia malengo na dhamira yake hiyo akitamka 'viliingia nyongo katikati ya safari' baada ya kuona anachokidai "Chadema hawakunipa ushirikiano kama mwanachama mwenzao."

INAENDELEA UK. 12

# Ripoti LHRC: Jinsia ina ahueni, ila kuna mengi bado ni shida




Mkurugenzi Mtendaji wa LHRC Anna Henga (katikati) na wadau wengine wa haki za binadamu walipozindua ripoti hiyo wiki iliyopita. **PICHA: SABATO KASIKA**

**Na Sabato Kasika**

KITUO cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), kimezindua ripoti yake ya haki za binadamu nchini ya mwaka 2021, iliyowekwa hadharani ikielezea mafanikio na changamoto katika kulinda haki hizo nchini.

Ripoti hiyo ilizinduliwa wiki iliyopita, jijini Dar es Salaam, ambayo Mkurugenzi Mtendaji wa kituo hicho, Anna Henga anafafanua mafaniko na magumu yaliyopitiwa.

Inasema, katika upatikanaji haki na jinai nchini mwaka jana, serikali na mahakama ziliendelea kuchukua hatua mbalimbali ikiwamo ujenzi na ukarabati wa majengo ya mahakama.

Henga anasema, hatua hiyo imeenda sambamba na uteuzi wa majaji wapya, kuajiri mahakimu na matumizi ya TEHAMA ili kuimarisha upatikanaji wa haki na utekelezaji wa mapendekezo yaliyopendekezwa ikiwamo upanuzi wa programu ya mahakama zinazotembea.

> Takwimu za polisi za mwaka 2021 zinaonyesha kuwa matukio ya ukatili dhidi ya watoto yalipungua kutoka 15,870 mwaka 2020 hadi 11,499 mwaka 2021.

"Pamoja na jitihada hizo za upatikanaji wa haki, utafiti huu umebaini kuwa upatikanaji wa haki unawindwa na changamoto kadhaa ikiwamo rushwa ambayo ndio ilitajwa kuwa kikwazo kikubwa zaidi na asilimia kubwa ya wananchi walioshiriki katika utafiti huu kwa asilimia 79," anasema.

Anasema kwa muda mrefu wa mashauri ya mahakamani, uelewa mdogo wa sheria miongoni mwa wananchi na gharama za uwakilishi wa kisheria, lugha ya mahakama na kisheria (Kiingereza), pia vinatajwa kuwa kikwazo.

"Takriban theluthi mbili ya wahojiwa, asilimia 62 walisema uhaba wa watumishi wa mahakama ni tatizo kwao katika suala la upatikanaji haki. Hivi sasa, Idara ya Mahakama inakabiliwa na upungufu wa wafanyakazi 4,728 sawa na asilimia 46, ambao umeathiri utoaji wa haki kwa wakati,"anasema.

Mkurugezi Mtendaji huyo anasema, katika hali ya haki ya jinai, mambo makubwa yaliyobainishwa kuwa ni changamoto kwenye utafiti wao, ni kuwekwa watu kizuizini muda mrefu kabla ya uchunguzi kukamilika.

"Ucheleweshaji wa upelelezi na kuahirishwa kwa kesi mara kwa mara, msongamano katika vituo vya polisi na magereza, matumizi mabaya na mianya ya mashauriano, ucheleweshaji wa kuwapeleka watuhumiwa mahakamani, ukiukwaji wa haki za wafungwa na mahabusu," anasema.

Anaongeza kwamba, lipo pia tatizo la ukosefu wa rasilimali za kutosha kwa ujumuishaji upya wa kijamii wa wakosaji waliowekwa rumande na kunyimwa dhamana kwa makosa yasiyo na dhamana.

"Ripoti hii inaangazia hali ya haki za makundi maalum kama vile wanawake, watoto, watu wenye ulemavu na wazee na inaonyesha kupungua kwa kiasi fulani kwa matukio ya ukatili dhidi ya wanawake na watoto. Hata hivyo tunahitaji kufanya juhudi zaidi kwani matukio bado ni mengi," anasema.

**AHUENI YA JINSIA**

Anasema, takwimu za polisi za mwaka 2021 zinaonyesha kuwa matukio 17,874 ya ukatili dhidi ya wanawake yaliripotiwa na kwamba hiyo ni pungufu ya matukio 8,670 yaliyoripotiwa kwa mwaka 2020.

"Takwimu za polisi za mwaka 2021 zinaonyesha kuwa matukio ya ukatili dhidi ya watoto yalipungua kutoka 15,870 mwaka 2020 hadi 11,499 mwaka 2021, ikiwa ni upungufu kwa asilimia 27.5," anasema.

Anataja haki zilizoripotiwa kukiukwa zaidi kwa mwaka wa 2021 zinajumuisha haki ya kuishi ambapo matukio yaliyoripotiwa yalijumuisha mauaji yanayotokana na wananchi kujichukulia sheria mkononi.

Pia, kuna mauaji ya imani za kishirikina na uchawi, mauaji ya wenza na masuala ya afya ya akili ambayo anasema yameendelea kuwa sababu ya vijana wengi kujiua.

"LHRC inatoa rai serikali, taasisi na jamii ya Watanzania kuendelea kulinda haki za binadamu na kuwawajibisha wale ambao wameshindwa kuheshimu haki hizo bila ubaguzi wa kikabila, kidini, kichama na kijinsia ili tuweze kuifikia jamii yenye haki na usawa," anasema.

## Aibuka na kuanika kilichompata safari ya Chadema, kurejea CCM

**INATOKA UK. 11**

''Nilitengwa kwa kila kitu ndani ya Chadema, sikupata ushirikiano wowote kama nilivyotarajia wakati namfuata Lowassa huko,'' anasema.

Anasimulia ni hatua iliyomfanya aamue kuondoka huko na kurudi alikotokea, CCM na bahati wakampokea kupitia Mkutano Mkuu wa chama, mjini Dodoma.

Kimsingi, anasimulia ulikuwa mkutano maalum kwa ajili ya kumchagua hayati Dk. John Magufuli kuwa Mwenyekiti mpya wa CCM Taifa, akipokea kijiti cha mstaafu, Jakaya Kikwete.

Msindai anasimulia kwamba kabla ya kuondoka Chadema, alimfuata Lowassa na kumueleza dhamira yake ya kuondoka huko, jambo ambalo anasema Lowassa anayemtaja kuwa rafiki yake, alimkubalia hata kumtakia heri anaporudi CCM.

Pia, anasimulia alivyorudi CCM, siku hiyo alipokelewa vyema, akisema aliamua kurudi CCM baada ya kuona wakati huo hapakuwa na kitu cha kupinga chini ya utawala wa hayati Magufuli kuchaguliwa kuwa rais wa mwaka 2015.

Hata hivyo, anakiri ugumu alioupata wakati wa kikao kilichompokea akipewa salamu ya kauli ambayo hatoisahau kisiasa akiinukuu: "Makada waliohama CCM na baadaye wakarudi ni sawa na ng'ombe waliokatwa mikia ndani ya kundi na kwamba ni rahisi wenzao kuwaona siyo wenzao kwa sababu muda wote wataonekana katika muonekano tofauti."

**ATWAA UENYEKITI CCM**

Pia, baada ya zama ubunge, Msindai alishakuwa Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM,) mkoa wa Singida na akapewa hadhi kuwa Mwenyekiti wa Wenyeviti wa CCM, Tanzania Bara.

Anajivuna alifanikiwa kuwaongoza wenzake baada ya kukabidhiwa kijiti hicho na aliyekuwa mtangulizi wake, Ali Mohammed Mtopa, aliyekuwa Mwenyekiti wa CCM mkoani Lindi.

Ilikuwaje akatwaa cheo hicho kikubwa? Anaisimulia Nipashe kwamba wenyeviti wenzake walimuamini na kumpa nafasi hiyo, kwa kuwa alikaa nao vizuri na hakuwahi kugombana nao kwa namna yoyote.

**ALIKOTOKEA KIMAISHA**

Mwanasiasa huyo alizaliwa mwaka 1948 mkoani Singida na kufanikiwa kusoma ngazi ya juu katika fani ya wanyamapori, kisha akaajiriwa serikalini kama Ofisa Wanyamapori katika mikoa mbalimbali, hadi alipostaafu na kuingia katika siasa.

Kwa sasa mwanasiasa huyo amestaafu siasa na kuamua kujishughulisha na shughuli za ufugaji nyumbani kwake jijini Mwanza.

**SIASA YA LEO?**

Msindai anaisifu CCM sasa imempata mtu sahihi, Abdulrahman Kinana, Makamu Mwenyekiti (Bara) atakayemsaidia Mwenyekiti Rais Samia Suluhu Hassan, kuendesha demokrasia ndani ya CCM, hata kushika vyema dhamana ya kuongoza nchi.

Msindai anamtaja Kinana kuwa mtu mwema anayejua siasa za utu, heshima na kuvumiliana,binafsi anamtaja anamfahamu kwa muda mrefu na atamsaidia Mwenyekiti Samia kukiboresha chama , CCM.

'Rais atapumzika sana, amechagua mtu sahihi kabisa! Mimi namfahamu Kinana ni rafiki yangu wa siku nyingi,'' anasema.

Pia, anamsifu Rais Samia kuwa anaongoza nchi kwa falsafa sahihi ambayo ni nzuri sana katika utendaji, akiwa makini dhidi ya wanaokosea.

Mwanasiasa huyo ana rai kwa rais kwamba, serikali inapolipa madeni ya wazabuni, kufungua milango ya ajira kwa sekta zote, kudumisha demokrasia na kuweka mkazo katika kilimo ni jambo muhimu, kwani ni kati ya mambo yanayogusa maisha ya wananchi, ambao pia ndio wapiga kura katika uchaguzi.

Pia anawashauri wabunge wajitume kutumikia wananchi, kwani kuna baadhi ya watu wanajisahau baada ya kuchaguliwa na kushindwa kutekeleza kinachowaweka katika nafasi hizo kupitia kura.

SIASA ZA KENYA;

# Zimejaa utatanishi kinachotawala kikuu ama ni sera au ukabila?

Na Mwandishi Wetu

KUANZISHWA muungano, umekuwa msingi wa siasa za Kenya tangu uchaguzi wa mwaka 2002. Katika uchaguzi wa mwaka 1992 na 1997, vyama vikuu vilifanikiwa kuchukua asilimia 60 ya kura dhidi ya chama tawala wakati huo , KANU kilichopata asilimia 35, japokuwa Kanu bado ilishinda.

Hatua hiyo ilizalisha muungano wa National Rainbow Coalition wakati wa uchaguzi wa 2002, muungano ulivileta pamoja vyama vyote vikuu vya upinzani wakati huo, dhidi ya mgombea wa chama cha KANU.


Katika uchaguzi wa mwaka 2007, mchuano wa kisiasa ulikuwa kati ya chama PNU cha Rais aliyekuwa madarakani Mwai Kibaki, ambacho kilikuwa muungano wa vyama vya kisiasa vinavyomuunga mkono na Orange Democratic Movement (ODM) chama cha kiongozi wa upinzani Raila Odinga, kilicholeta pamoja watu mashuhuri waliowakilisha makabila tofauti nchini humo.

Uchaguzi wa mwaka 2013 uliimarisha msingi wa ujenzi wa muungano miongoni mwa vyama tofauti vya kisiasa.

Katika uchaguzi huo maalum, Chama cha National Alliance Party (TNA) cha Rais Uhuru Kenyatta na United Republican Party (URP) cha William Ruto, viliunda muungano dhidi ya Muungano wa Mageuzi na Demokrasia (CORD), uliowaleta pamoja Raila Odinga wa chama cha Orange Democratic Party of Kenya (ODM) na Kalonzo Musyoka, wa Wiper Democratic Movement.

Uchaguzi wa 2017, pia ulikuwa na ushindani mkali kati ya chama tawala cha Jubilee, uliokuwa muungano wa vyama vyote vilivyounga mkono Rais Uhuru na chama cha National Super Alliance (NASA), uliokuwa muungano wa vyama vilivyounga mkono mpinzani Raila.

Hivyo, katika siasa Kenya, kuundwa muungano ni hatua nyeti ya kuhakikisha washirika wa uchaguzi uliopita hawatupwi mbali, kwa lengo la kuingiza washirika wapya.



Rais Uhuru Kenyatta wa Kenya, alipokutana na viongozi wenza wa kisiasa mwaka jana, Raila Odinga na wakuu wa muungano wa One Kenya Alliance (OKA), Ikulu mjini Mombasa. **PICHA: MTANDAO**

### UCHAGUZI UJAO

Unapokaribia Uchaguzi Mkuu ujao mwezi Agosti, muundo wa kisiasa au miungano inachukua mtindo kama ya awali. Hapo inafafanuliwa, muungano wa uchaguzi wa 2017 wa NASA na Jubilee, haujaweza kusimamia vizuri muungano wa wahusika wapya.

Muungano wa NASA, kati ya washirika wanne wakuu wawili (Musalia Mudavadi na Mosses Wetangula) walijiondoa katika muungano wa NASA na wanaunga mkono Naibu Rais William Ruto katika Muungano wa Kenya Kwanza.

Pia, mshirika mwingine mkuu,Kalonzo Musyoka hadi hivi karibuni alikuwa kwenye Muungano wa One Kenya, kabla ya kujiunga tena na Azimio One Kenya.

Chama cha Jubilee, chenyewe kilikuwa muungano wa vyama vingi, pia kimegawanyika kwa sababu ya mpasuko kisiasa kati ya Rais Uhuru na Naibu wake Ruto.

Rais Uhuru ameanika anamuunga mkono aliyekuwa mpinzani wake NASA, Raila chini ya muungano wa Azimio la Umoja, huku naibu akiunda muungano mpya chini ya bendera ya Kenya Kwanza.

Muungano wa Azimio ulileta pamoja chama cha ODM cha Raila, Wiper cha Kalonzo, Jubilee cha Uhuru, KANU ya Gideon Moi, NARC ya Charity Ngilu, Prof. Kibwana pamoja na vyama vingine vingi kote nchini; huku muungano wa Naibu Rais William Ruto Kenya Kwanza ukileta pamoja UDA , chama cha ANC cha Musalia Mudavadi, FORD-K ya Mosses Wetangula pamoja na vyama vingine vingi kutoka eneo la kati la Kenya.

### NI SERA AU MASLAHI?

Muungano wa vyama vya kisiasa nchini Kenya kwa kiasi kikubwa una uhamasishaji wa kikabila, kupitia kuunganishwa kwa wanaochukuliwa kuwa viongozi wa makabila, sera haina nguvu sana.

Makabila huangalia wapi viongozi wake wanaangaziwa vyema ndani ya chama au muungano wa vyama kama mshawishi mkuu wa jinsi ya kupiga kura.

Ugawaji nafasi muhimu kwa viongozi wa makabila wanaotambulika, na chini ya kipengele muhimu katika uundaji muungano, mara tu maslahi makuu ya mtu binafsi yanapofikiwa basi maslahi ya jamii yanachukuliwa kuwa yametolewa.

Kwa upande wa Azimio, kwa kukidhi matakwa kibinafsi ya Kalonzo Musyoka, wapiga kura wa kabila la Akamba kutoka eneo la Mashariki wanahisi kuridhika na kwa uwezekano mkubwa wangempigia kura Raila, ambaye ndiye mgombea wa urais wa Azimio.

Hivyo basi, kuridhika kwa viongozi hao wa makabila, imekuwa kigezo muhimu katika uundwaji muungano wa kisiasa nchini Kenya.

### UAMUZI MAHAKAMA JE?

Uamuzi wa Mahakama ya juu zaidi mnamo mwezi Machi 31 ulibatilisha mpango wa BBI, umetoa nafasi kubwa katika muungano wowote unaoundwa kwa msingi wa kugawana mamlaka.

Mchakato wa BBI, ulikuwa ni jaribio la kupanua mamlaka ya utendaji wa kitaifa kupitia kuanzishwa kwa nyadhifa kama vile Waziri Mkuu na Naibu Waziri Mkuu, ambazo zingesaidia katika kuzawadia jamii tano kubwa nchini kinyume na nyadhifa mbili za Rais na Naibu Rais zilizopo kwa sasa.

Kuundwa nyadhifa hizo za ziada kungehakikisha kuwa kuna mpangilio mpana zaidi wa ugavi wa mamlaka ndani ya muungano wowote utakaoundwa.

Katika maandalizi ya uchaguzi wa 2022 nafasi ya Mgombea Mwenza na Naibu Rais aliyefuata (ikiwa ameshinda) ilikuwa imeshuka thamani kwa sababu ya unyanyasaji na kushushwa kwa hadhi na ofisi ya sasa ya Rais Uhuru Kenyatta.

Naibu Rais kwa kipindi cha miaka minne iliyopita amejipata nje katika serikali ambayo alikuwa mchangiaji mkubwa katika muundo wake.

Hata hivyo kutokana na kushindwa kwa pendekezo lililotarajiwa la BBI, nafasi ya mgombea mwenza itachukua jukumu kubwa sana katika muungano wowote utakaoundwa; anayepata nafasi hiyo atalazimika kuwa na mchango mkubwa katika jinsi kabila lake litakavyopiga kura.

> Rais Uhuru ameanika anamuunga mkono aliyekuwa mpinzani wake NASA, Raila chini ya muungano wa Azimio la Umoja, huku naibu akiunda muungano mpya chini ya bendera ya Kenya Kwanza.

Hivi sasa, miungano yote miwili ya Azimio na Kenya Kwanza inakabiliwa na mtanziko wa mgombea mwenza; kwa upande wa Azimio, swali muhimu ni iwapo muungano wa zamani kati ya Raila/Kalonzo ndio utakaowasilishwa na hivyo kuhatarisha kuwatenga washirika wapya walio na idadi kubwa ya upigaji kura ambayo imeletwa na Rais Uhuru Kenyatta, au muungano huo utaangazia kadi ya jinsi ya kike ambayo pia itatoka mlima Kenya?

Hili naamini ndilo tatizo la kisiasa ambalo muungano wa Azimio unapaswa kulishughulikia tunapoelekea Uchaguzi Mkuu wa Agosti 2022.

Kwa upande wa muungano wa Kenya Kwanza, uongozi wake umekuwa ukisisitiza kwamba haukuegemea kwenye mgao wa nafasi kwa wachache, badala yake, ulikuwa wa kutatua changamoto za kiuchumi za siku nyingi zinazoikabili nchi na kwamba nafasi ya mgombea mwenza haikuwa na umuhimu wowote.

Hata hivyo kandokando kumekuwa na fununu kwamba vinara wake wakuu walikuwa wanahifadhi nafasi hiyo kwa wapiga kura wake wengi kutoka mlima Kenya.

Tangu kuingia siasa za vyama vingi nchini Kenya mwaka 1992, uchaguzi Mkuu wa 2022 utakuwa ni uchaguzi wa kwanza eneo la Mlima Kenya halitakuwa na mwanasiasa anayewania nafasi ya rais wa jamhuri, na hivyo Muungano wowote wa kisiasa unaoundwa utalazimika kutilia maanani muhimu wa eneo hilo lenye wapiga kura wengi.

Hivyobasi Muungano wowote utalazimika kutoa wadhfa huo kwa eneo hilo kwa lengo la kuvutia wapiga kura wake.

• *Kwa mujibu wa BBC*

JUKWAA LA VIONGOZI

# Rais Mobutu wa Zaire na safari alikotoka, kutumika hadi kuishia

Na Christina Mwakangale

WENGI wanaomjua, wanamtambua kwa jina, Mobutu Seseko Wazabanga Kuku. Lakini akifuatuliwa alikotokea, tangu utotoni jina lake maarufu ni Joseph Mobutu na ndilo alilotambulika nalo.

Kwa mtindo wake wa mavazi ya chui, hasa kofia ambayo ni nadra kumkuta ameivua. Alikuwa mtu wa misimamo mikali na msimamizi, mwamuzi wa jambo lake mwenyewe, hata akajibadili jina mwenyewe mwaka 1972 na kujiita Mobutu Sese Seko.

Huko nyuma alikuwa Msaidizi Mkuu wa Jeshi wa Waziri Mkuu Patrice Lumumba na kuna wakati akajipandisha cheo chake kijeshi, kutoka sajini hadi luteni kanali.

Kimaisha, Mobutu alikuwa msingi wa vitendo na maarifa ya kawaida. Walinzi wa Umoja wa Mataifa au wananchi walipokamatwa na askari wa Lumumba, Mobutu alikuwa ndio kimbilio la Umoja wa Mataifa, kuweka mambo sawa, hata ikafika hatua ya kumuamini sana.

Alionekana kuwa mtu wa fikra sahihi ambaye hata watu waliamini kuwa analinda maslahi ya taifa changa.

Mnamo Septemba ya mwaka 1960, baada ya Rais Joseph Kasavubu kumfukuza kazi Lumumba, huku Lumumba naye akidai kumfuta kazi Rais Kasavubu, uvumi ulienea mji wa Leopoldville na Umoja wa Mataifa akisakwa kwa msaada.

Bila kutarajia, Kanali Joseph Mobutu akiwa amevalia mavazi ya kiraia alifika mbele ya umati wa watu akiuomba Umoja wa Mataifa umsaidie kuondoka nchini humo, akidai amechoka.

Mkuu wa Operesheni za Umoja wa Mataifa nchini humo wakati huo, Rajeshwar Dayal, akamsihi Mobutu asiondoke bali asalie kusaidia nchi yake.

Siku mbili baadaye Mobutu akiwa na sare za jeshi alifika makao makuu ya ofisi za Umoja wa Mataifa, Leopoldville, akidai kuchoka na makelele na anataka sehemu tulivu. Na wakamsikia, akawekwa ndani ya chumba cha mtumishi mmoja wa UN, akipatiwa pombe kali huku akisikiliza radio.

Alionekana kufurahia muziki wa mtindo wa Chacha, ghafla radio Leopoldville ikanyamaza kuchezesha muziki na sauti ikatoka ikitangaza kusimamishwa kwa Rais, Waziri Mkuu na Bunge na kwamba mtu huyo anayetangaza ndiye amechukua nchi.

"Ni mimi, Mobutu alisikika akisema, akaruka kwa ushindi na kuelekeza kidole kwenye radio.. 'ni mimi!.'

Brian Urquhart, mtu aliyempatia chumba apumzike, alishikwa na hasira akimweleza Mobutu kuwa, kama ni sehemu ya kutangaza mapinduzi ya kijeshi ni mitaani na wafuasi wake na si kwenye chumba chake cha kulala.

Mobutu aliondolewa pale na yasemekana kitendo alichofanya kilipatiwa nguvu na Marekani na hakikuwa cha kikatiba.



Marehemu Rais Mobutu Seseseko Wazabanga Kuku. **PICHA: MTANDAO**

> Daima vazi lake tambulishi la kofia ya ngozi ya chui na ndege yake Boeing 747 inayobeba ujumbe wake.

Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa wakati huo, Dag Hammarskjold na wawakilishi wake Congo walikataa kumtambua kuwa ni rais.

Mabalozi wa Marekani na Uingereza, huko Leopoldville walipinga uamuzi wa UN, wakisema Mobutu alikuwa si mkomunisti na anafaa kwa kuongoza Congo.

Mobutu alibadili jina lake na kujiita Mobutu Sese Seko Kuku Ngbendu akimaanisha, 'Mpiganaji anayeshinda kila vita na kuacha moto kila apitapo au jogoo asiyeacha kuku jike peke yake'. Daima vazi lake tambulishi la kofia ya ngozi ya chui na ndege yake Boeing 747 inayobeba ujumbe wake.

Brian anasema, walikutana uso kwa uso wakati wa hafla moja, ambapo Mobutu alikumbuka urafiki wao mwanzoni kabisa mwa uhuru wa Congo, akisema kuwa Brian hakuwa mwema mara ya mwisho walipokutana.

Mwaka 1997, Mobutu alipofariki dunia kutokana na saratani, nchi yake ilikuwa katika sintofahamu na mapinduzi yalimweka madarakani Laurent Kabila.

Baada ya Umoja wa Mataifa kufanikiwa kuondoa jeshi la Ubelgiji kutoka Katanga, wanamgambo wa Tshombe walikuwa ni maofisa wa Ubelgiji ambao walikuwa ni askari kanzu na mamluki wengineo kutoka vikosi vya parachuti vya Ufaransa huko Algeria.

Katanga ikiendelea kuwa imejitenga, maeneo mengine ya nchi hayakuwa tulivu na wengi serikalini na hata ndani ya Umoja wa Mataifa walipinga kujitenga kwa jimbo hilo, ilikuwa ni lazima kupata suluhu.

### SAFARI YA MAISHA YAKE

Mobutu Sese Seko alizaliwa Oktoba 14 mwaka 1930. Huyo ni mzaliwa wa Congo, akiwa mwanasiasa na ofisa wa jeshi.

Ameiongoza Congo kuanzia mwaka 1965 hadi 1971 na baadae nchi hiyo ikaitwa Zaire, bado chini ya uongozi wake hadi alipokoma 1997.

Alihudumu kama Mwenyekiti wa Jumuiya ya Umoja wa Afrika (Chairman of the Organisation of African Unity), kuanzia mwaka 1967 hadi 1968.

Kipindi cha mgogoro wa Congo Mobutu, alihudumu kama Amiri Jeshi Mkuu, akipewa usaidizi na Ubelgiji na Marekani na ndipo alipoiondoa serikali iliyochaguliwa kidemokrasia ya mzalendo, mwenye mrengo wa kushoto, Patrice Lumumba mwaka 1960.

Serikali yake ilipanga kunyongwa kwa Lumumba mwaka 1961 na kuendelea kuongoza majeshi ya nchi hiyo hadi alipochukua madaraka moja kwa moja kupitia mapinduzi ya pili mwaka 1965.

Ili kuimarisha mamlaka yake, alianzisha chama chake kiitwacho Popular Movement of the Revolution' chama pekee cha kisheria cha kisiasa mwaka 1967, akabadilisha jina la Congo kuwa Zaire mwaka 1971.

Msaada mkubwa wa kiuchumi kutoka China uliingia Zaire na ulimpa Mobutu mabadiliko zaidi katika shughuli zake na serikali za Magharibi, hadi kujitambulisha kama "mwanamapinduzi anayepinga ubepari", na kumuwezesha kuepuka kwenda kwenye Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) kwa ajili ya msaada.

Ilipofika mwaka 1990, kuzorota kwa uchumi na machafuko Zaire, yalimfanya Mobutu akubali kugawana madaraka na viongozi wa upinzani, lakini alitumia jeshi kuzuia mabadiliko hadi Mei 1997, wakati vikosi vya waasi vikiongozwa na Laurent-Désiré Kabila vilipotawala nchi na kumpeleka uhamishoni.

Alienda uhamishoni wakati tayari anaugua saratani ya tezi dume, alifariki dunia miezi mitatu baadaye, mjini Rabat nchini Morocco.

• ***Kwa mujibu wa taarifa mbalimbali.***





# Familia yaomba msaada makazi

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

FAMILIA ya watu sita inayoishi Mtaa wa Oysterbay, Kata ya Makulu jijini Dodoma, imeomba serikali kuwasaidia baada ya kuachwa bila makazi kutokana na nyumba waliyokuwa wakiishi kubomolewa huku chanzo kikidaiwa ni ujenzi holela.

Akizungumza jana na Nipashe, Kibinda Mwoghu, ambaye ni baba wa familia hiyo, alisema kubomolewa kwa nyumba hiyo kumesababisha hasara ya Sh. milioni saba ikiwemo familia yake kukosa makazi.

Mwoghu alisema nyumba hiyo ilibomolewa na mwenyekiti wa serikali ya mtaa huo kwa kushirikiana na askari mgambo kutoka jiji.

Alisema ubomoaji wa nyumba yake ulifanyika akiwa ametoka ndipo mwenyekiti akaja na mgambo wakabomoa bila taarifa yoyote hali iliyosababisha kuishi nje hadi sasa.

Mwoghu alisema wamekuwa katika mgogoro na mwenyekiti wake kwa muda mrefu baada ya kupimiwa viwanja vyake na kukuta viko zaidi ya kimoja hivyo alitakiwa atoe kiwanja kimoja baada ya kukaidi ndio yakaanza malumbano hayo.

Alisema baada ya kutokea kwa tukio hilo, alikwenda kutoa taarifa katika kituo cha polisi cha Chimwaga na mwenyekiti huyo aliitwa ambapo alisema wanaendelea kusubiri hatua zinazofuata.

"Wanadai kuwa tumejenga karibu na korongo lakini tupo wakazi wengi tu. Ninachojiuliza kwa nini wabomoe nyumba yangu peke yangu halafu anavizia wakati sipo. Hili suala limeniathiri sana na kunirudisha nyuma naomba serikali iingilie kati," alisema.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Mtaa huo Samson Ndama alikiri kutokea kwa tukio hilo na kusema lilitekelezwa na mgambo kutoka jiji chini ya kikosi cha udhibiti ujenzi holela.

Alisema mhusika ameshapewa taarifa mara kadhaa kusitisha ujenzi eneo hilo lakini hakusikia hivyo baada ya kuonywa ndipo mgambo hao waliamua kuchukua uamuzi wa kumbomolea nyumba yake.

"Ni kweli amebomolewa nyumba yake kutokana na kukaidi agizo la serikali la kumtaka kusitisha ujenzi lakini alikiuka na mimi kazi yangu ni kuongoza askari wanapomhitaji mtuhumiwa ambaye anapatikana katika mtaa wangu,"alisema.

# Watendaji afya watakiwa kuongeza kasi kuhamasisha uchangiaji damu

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imewataka watendaji wa sekta ya afya nchini kuboresha usimamizi katika uhamasishaji uchangiaji damu salama ili kukidhi mahitaji ya huduma hiyo.

Naibu Waziri wa Afya, Dk. Godwin Mollel, alisema hayo juzi aliposhiriki kwenye kikao kazi cha kujadili uboreshaji wa uendeshaji usimamizi wa huduma za damu salama nchini kilichowakutanisha waganga wakuu wa mikoa Tanzania Bara na watendaji wa Mpango wa Taifa wa Damu Salama.

"Tumeona kuna shida kubwa ya damu. Damu haiuzwi wala kutengenezwa na ili tupate damu ni lazima tuhamasishe watu watoe damu," alisema.

Pia alisema wamekutana ili wajadiliane na kuweka mikakati bora ya kuboresha ukusanyaji wa damu salama pamoja na kujengeana uwezo na kubadilishana uzoefu katika kuhamasisha zaidi jamii kuhusu uchangiaji damu.

Dk. Mollel alisema kipaumbele cha Wizara ya Afya ni kuboresha huduma hizo nchini kwa kuhakikisha wananchi wanapata huduma ya uhakika na iliyo bora, hivyo upatikanaji wa damu salama ni ajenda muhimu katika kufikia malengo ya wizara.

"Tubadilishane uzoefu wa namna wataalam wenzetu kwenye kanda zetu nane za damu salama wanavyofanya kazi ikiwa ni pamoja na kusaidiana rasilimali zilizopo na kuhakikisha tunakusanya damu salama kwa kiwango kikubwa zaidi," alisema Dk. Mollel.

Aidha, alishauri Mpango wa Taifa wa Damu Salama kuendelea kutambua mchango wa wachangiaji damu na kuwa nao karibu ikiwa ni pamoja na kuwasadia pindi wanapohitaji huduma za damu salama.

Meneja wa Mpango wa Taifa wa Damu Salama, Dk. Magdalena Lyimo, alisema lengo la serikali ni kuhakikisha huduma za damu salama zinapatikana wakati wote ili kufanikisha azma ya serikali kukusanya damu salama ili kutosheleza mahitaji ya nchi.

"Damu salama ni nguzo muhimu ya utoaji wa huduma za afya. Ili kukidhi mahitaji ya damu hapa nchini tunapaswa kukusanya chupa 550,000 za damu sawa na asilimia moja ya idadi ya wananchi," alisema.

Dk. Lyimo alisema kwa mwaka 2020/21 walikusanya chupa 330,000 sawa na asilimia 60 ya mahitaji, hivyo kuwa na uhaba wa asilimia 40 sawa na chupa 220,000 za damu.

"Kikao hiki kimeitishwa sasa ili kujadiliana na kuweka mikakati madhubuti ya kuhakikisha tunaziba hilo pengo la asilimia 40 na kufikisha idadi ya chupa 550,000 za damu kwa kuongeza hamasa zaidi ya uchangiaji damu pamoja na kuendelea kuelimisha jamii juu ya umuhimu wa kuchangia damu" alisisitiza.

Mkurugenzi wa Huduma za Tiba katika Wizara ya Afya, Dk. Omary Ubuguyu, aliahidi kuboresha usimamizi wa mikakati iliyowekwa ya ukusanyaji damu na kuwataka wataalamu wa afya katika vituo vya kutolea huduma kufanyia kazi maelekezo yote yanayotolewa na viongozi ikiwa ni pamoja na kuboresha huduma kwa wateja sambamba na kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora.



Baadhi ya wabunge wakiingia bungeni jijini Dodoma jana, kuhudhuria mkutano wa saba wa Bunge, kikao cha nane, baada ya mapumziko ya Sikukuu ya Pasaka. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Askofu ataka umakini matumizi chakula

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

WAKULIMA wa mikoa ya Kanda ya Kati wameshauriwa kuhifadhi chakula cha kutosha kutokana na uhaba wa mvua ambao unatishia baa la njaa katika msimu huu wa kilimo.

Pia wametakiwa kutotumia chakula hicho katika matumizi yasiyo na tija ikiwamo upikaji pombe za kienyeji zinazotumia nafaka kama vile mahindi na mtama.

Mwenyekiti wa Jumuiya ya Maridhiano Mkoa wa Dodoma, Askofu Dk. Evance Chande, alitoa ushauri huo juzi alipokuwa akitoa salamu zake za Sikukuu ya Pasaka kwa waumini wa Kanda ya Kati.

Askofu Chande alisema kutokana na kiwango kidogo cha mvua zilizonyesha kwa baadhi ya mikoa ikiwamo ya Kanda ya Kati, wakulima wanapaswa kuhifadhi chakula na kuepuka matumizi yasiyo na tija ambayo yanayoweza kusababisha uwapo wa njaa.

Katika salamu zake hizo, aliwaomba Watanzania kuendelea kukemea vitendo vya rushwa vinavyofanywa na baadhi ya viongozi wa ngazi mbalimbali wasiokuwa na hofu ya Mungu na kusababisha kukwamisha shughuli mbalimbali za kimaendeleo.

Alisema pamoja na juhudi mbalimbali zinazofanywa na serikali katika kukomesha rushwa, Watanzania wenyewe wanaweza kuwa msaada mkubwa katika kuwafichua na kukemea tabia hiyo ambayo imekuwa inarudisha nyuma maendeleo ya wananchi.

Pia aliwataka Watanzania kutoilaumu serikali juu ya upandishaji wa bidhaa mbalimbali nchini bali kinachotakiwa ni kuomba mbele za Mungu ili hali hiyo iondoke kama ilivyo kuwa katika janga la UVIKO-19.

"Tatizo hili la upandishaji wa bei wa bidhaa mbalimbali halipo hapa nchini Tanzania pekee bali karibu nchi nyingi duniani vitu vyao vimepandishwa bei, hivyo hakuna haja ya kuilalamikia serikali yetu," alisema.



# Watoto mazingira magumu wasaidiwa vifaa vya elimu

**Na Nebart Msokwa,**
MAKETE

ZAIDI ya watoto 400 wanaoishi kwenye mazingira magumu wa Tarafa ya Matamba, wilayani Makete mkoani Njombe, wamenufaika na msaada wa kununuliwa vifaa vya shule pamoja na sare katika kipindi cha miaka sita.

Walionufaika na msaada huo ni kutoka kwenye shule saba za msingi za tarafa hiyo ambao wananunuliwa madaftari, sare za shule, viatu, soksi, sweta, mikebe na peni, kalamu za risasi kwa wanafunzi wa darasa la kwanza na la pili.

Misaada hiyo inatolewa na Shirika lisilokuwa la kiserikali la Maria Foundation lenye makao makuu yake Uyole, jijini Mbeya ambalo mwanzilishi wake ni Yoab Mhavile, raia wa Marekani mwenye asili ya Kijiji cha Matamba wilayani Makete.

Mwakilishi wa Shirika hilo, Haruni Mhavile alisema mwanzilishi wa shirika hilo aliamua kuanzisha shirika hilo ili kuwasaidia wanafunzi wanaotoka kwenye mazingira magumu kwa sababu hata yeye alisoma kwenye mazingira hayo.

Alisema walifanya utafiti wakabaini kwamba wanafunzi wengi huwa wanaacha shule ama kutofanya vizuri kutokana na kukosa mahitaji muhimu ya shule na ndiyo maana waliamua kuwasaidia.

"Tulianza na shule moja ya msingi, Matamba, sasa hivi tumeongeza shule sita na tutaendelea kupanua wigo ili tuzifikie shule zote za tarafa hii, tunaamini kwamba miongoni mwa hawa tunaowasaidia wanaweza wakawa viongozi wakubwa wa kulisaidia taifa," alisema Mhavile.

Alisema ili kuwapata watoto wenye sifa za kusaidiwa, wanasaidiana na baadhi ya walimu wa shule hizo ambao huwafuatilia kila mtoto familia anayotoka.

Baadhi ya walimu wa shule zinazonufaika na msaada huo walilishukuru shirika hilo kuwa limeongeza mahudhurio ya wanafunzi shuleni kwa kuwa baadhi yao huwa wavivu kwa sababu ya kukosa mahitaji muhimu.

Mwalimu Mkuu Msaidizi wa Shule ya Msingi Kisaula, Iman Kiswaga, alisema mara nyingi watoto wanaotoka kwenye mazingira magumu, wanakosa vifaa kutokana na walezi wao kutokuwa na uwezo wa kununua.

Alisema baada ya shirika hilo kuanza kuwasaidia wanafunzi wamekuwa na uhakika wa kuhudhuria shuleni wakiwa na vifaa vyote vya kuwawezesha kusoma vizuri.

"Ili mwanafunzi akamilike anatakiwa kuwa na vifaa vyote, sasa hawa watoto wengi ni wadogo ambao hata utunzaji wa vifaa hivi huwa ni mdogo, unaweza ukakuta leo ana daftari jipya kesho hana, sasa wazazi wengine huwa wanashindwa kumudu kuwanunulia kila siku," alisema Kiswaga.

Akizungumza kwa niaba ya wazazi, Mjumbe wa Kamati ya Shule ya Msingi Kisaula, Modestus Mboka, alisema msaada huo utasaidia kuboresha sekta ya elimu kwenye shule ambazo zipo kwenye tarafa hiyo.

Alisema msaada huo utasaidia kuongeza kiwango cha ufaulu kwa wanafunzi na miongoni mwao wengine ni yatima na hawana watu wa kuwasukuma kuwa na mwamko wa elimu.



Mwakilishi wa Shirika lisilo la kiserikali Maria Foundation, Haruni Mhavile (kushoto), akikabidhi msaada wa vifaa mbalimbali vya shule. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## MUST yaanzisha mkakati kuwatafutia vyuo wanafunzi wenye vipaji nje ya nchi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SERIKALI ya wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST), imeanzisha mkakati maalumu wa kuwaibua wanafunzi wenye vipaji chuoni hapo na kuwaendeleza kwa kuwatafutia fursa nje ya chuo hicho.

Imeanzisha tamasha maalumu la vipaji ambalo litakuwa linafanyika kila mwaka na wanafunzi wenye ubunifu mbalimbali wanaonyesha na kushindanishwa na kutangaza ubunifu wao ambao utaendelezwa kwa ajili ya kuwainua kiuchumi.

Rais wa Serikali ya wanafunzi hao, Aman Kamdeka, aliyasema hayo juzi wakati wa tamasha la kwanza la vipaji lililofanyika chuoni hapo na kuwashirikisha wanafunzi wote wanaosoma chuoni hapo.

"Tumeanzisha tamasha hili kwa sababu tumebaini kuwa wapo wanafunzi wenye ubunifu, lakini hawana ujuzi wa namna ya kujiendeleza kupitia ubunifu wao, sasa tunaamini kwamba kupitia tamasha hili vipaji hivyo vitaonekana," alisema Kamdeka.

Alisisitiza wanafunzi wanaoibuliwa kupitia tamasha hilo wanaweza kuutumia ubunifu wao kujiinua kiuchumi na kujiajiri kupitia ubunifu huo badala ya kutegemea kuajiriwa.

Baadhi ya wanafunzi hao walisema tamasha hilo litawasaidia kutangaza ubunifu wao na kujipatia fedha kwa kuuza vitu ambavyo wanabuni na kuwasaidia hata kuboresha baadhi ya shughuli kwenye jamii.

Mmoja wa wanafunzi hao, Alexander Maganga alisema katika chuo hicho wapo watu waliobuni vitu mbalimbali vya kisayansi, lakini kutokana na sehemu za kuonyesha kuwa chache wanashindwa kunufaika.

Alisema wapo ambao wamebuni zana za kilimo, mashine za kuchakata mazao na baadhi wamebuni mashine za kukoboa na kupiga nafaka mbalimbali, lakini kutokana na kukosekana kwa maeneo ya maonyesho wanashindwa kuzitangaza.

# Wafuata maji mbali kisa mradi kuhujumiwa

**Na Nebart Msokwa,**
BUSOKELO

WANANCHI wa Kata ya Isange katika Halmashauri ya Busokelo, wilayani Rungwe, mkoani Mbeya, wamesema wanalazimika kutembea umbali mrefu kwenda kutafuta huduma ya maji kutokana na mradi uliojengwa na serikali kudaiwa kuhujumiwa.

Wananchi hao wanadai kuwa tangi la maji lililojengwa na serikali kwa ajili ya kuwahudumia linajaa mchanga na kusababisha maji kutowafikia kwenye maeneo yao na kulazimika kwenda kuchota kwenye mito.

Wananchi hao walitoa malalamiko hayo juzi wakati wa ziara ya mbunge wa jimbo hilo, Atupele Mwakibete, ambaye pia ni Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi na waliiomba serikali kuwasaidia kuondoa kero hiyo.

Mmoja wa wananchi hao, Julius Mwasomola, alisema katika vijiji vyao walifungiwa mabomba, lakini hayatoi maji na wataalamu hawajawahi kujitokeza kwenda kuwarekebishia hali inayosababisha kero kwao.

Alimuomba Naibu Waziri kuwahimiza wataalamu wa maji kuwarekebishia miundombinu ili waanze kupata huduma kama ilivyokuwa awali walipokuwa wameunganishiwa huduma hiyo.

"Hata wanafunzi wetu wanapata shida sana, wanahangaika kwenda kuchota maji mtoni, sasa huku kwetu dhana ya kumtua mama ndoo bado haijaonekana," alisema Mwasomola.

Diwani wa Kata ya Isange, Elias Mwasandele, alisema tangi la maji lililojengwa kwenye kata hiyo lilikuwa limejaa mchanga na sasa hivi wameamua kuajiri vijana ambao wanatoa mchanga huo ili kuruhusu kuingia.

Alisema mpaka sasa vijana hao wametoa zaidi ya malori 10 ya mchana na bado wanaendelea kutoa na kwamba hali hiyo imesababisha wananchi kutonufaika na mradi huo.

"Waliniambia kesho (jana) ndiyo wanaenda kumalizia kutoa ule mchanga na wakimalizia tutaanza kupata maji kwenye vituo vyetu, lakini tatizo hilo linaashiria kwamba mradi hauko vizuri," alisema Mwasandele.

Alimuomba Naibu Waziri kuwasaidia kuweka msukumo ili mradi huo urekebishwe kwa kuondoa matatizo yanayosababisha tangi hilo kujaa mchanga.

Akijibu malalamiko hayo ya wananchi, Naibu Waziri Mwakibete, aliahidi kufuatilia jambo hilo na kuhakikisha huduma ya maji inapatikana kwenye maeneo ya jirani na makazi ya wananchi kama ilivyo lengo la serikali.

Alisema pamoja na miradi hiyo ya maji, pia atahakikisha anashirikiana na viongozi wengine wa serikali katika wilaya hiyo kuhakikisha miradi mbalimbali ya maendeleo inaboreshwa ili kurahisisha upatikanaji wa huduma.

Alisema katika kipindi chake cha uongozi atahakikisha anatekeleza ahadi zote alizowaahidi wananchi wakati wa kampeni na wakati wa mikutano mbalimbali aliyoifanya baada ya kuchaguliwa.

Alisema kwa sasa yeye baada ya kuteuliwa na rais kuwa Naibu Waziri ameongezewa majukumu ambayo yanamfanya atumike kitaifa tofauti na ilivyokuwa awali.

"Sisi kazi yetu ni kumsaidia rais kuhakikisha wananchi mnapata huduma bora, sasa mimi kama mbunge wenu nitahakikisha mnapata miundombinu muhimu kwa ajili ya kurahisisha upatikanaji wa huduma," alisema Mwakibete.





## Zanzibar kuwa mwenyeji maadhimisho Wiki ya Afrika

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

ZANZIBAR inatarajia kuwa mwenyeji katika kupokea wageni wa nchi 54 za Afrika watakaoshiriki maadhimisho ya wiki ya Afrika Mei 22 hadi 29, mwaka huu.

Mwenyekiti wa chama cha waongozaji watalii (ZATO), Hassan Ali Mzee, alisema hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu maadhimiisho hayo.

Alisema Mei 25 ni siku ya Afrika na wataitumia wiki hiyo kwa kungana na mataifa mengine ya Afrika kujadili mambo mbalimbali ikiwamo mila, silka na tamaduni zao. Alisema kuna vitu ambavyo waafrika wanajivunia na kongamano hilo litajumuisha viongozi wastaafu barani Afrika akiwamo Rais mstaafu wa Nigeria, Olesegun Obasanjo, Rais mstaafu wa Botswana na Rais wastaafu wa Zanzibar, Dk. Amani Abeid Karume na Dk. Ali Mohammed Shein.

Aliwataja viongozi wengine wanaotarajiwa kushiriki kongamano hilo kuwa Dk. Jakaya Kikwete, Balozi Asha Rose Migiro, Amina Salum Ali na Balozi Mahomoud Thabit Kombo.

Alisema kando ya kongamano hilo kutafanyika kikao cha kamati ya amani na usalama na kubainisha kwamba mambo yatakayojadiliwa yanatokana na hali ya amani na utulivu iliyopo Zanzibar na ukarimu wa watu wake.

"Siku ya Kongamano tutaweka historia ya aina yake kwani Ngalawa zitabeba bendera za nchi 54 za Afrika kutoka Forodhani hadi hoteli ya Verde kwani hii ni kwa mara ya kwanza itafanyika hapa kwetu," alisema.

Alisema kongamano hilo lina lengo la kuwaunganisha watu na kuwaweka pamoja katika masuala ya utamaduni biashara mila na kutengeneza uhusiano baina ya nchi hizo na kunufaika na mahusiano hayo.

Akizungumzia wiki hiyo alisema ilianzishwa na muunganiko wa viongozi wa Afrika kwenye miaka 50 na 60 baada ya ukombozi walibuni jambo hilo la waafrika kukutana na kufanyika mara ya kwanza Senegal miaka 60 na 77 nchini Nigeria.

Alisema wameona upo umuhimu wa kurejesha jambo hilo kwa ajili ya kuwakutanisha waafrika kwa lengo la kujuana kutambuana kimila, kiutamaduni na kibiashara na muziki.

Pia kutakuwa na tamasha la biashara na wanategemea kupokea wageni 5,000 hadi 1,000 na aliwahamasisha watu wenye kazi za vikundi kushiriki na kujitangaza ili waweze kupata soko.

Aliwaomba wananchi kushiriki kwa wingi na wiki hiyo itakuwa inaizungumzia kwa kiasi kikubwa historia ya Zanzibar na watu wake.

# Mwinyi aipongeza India kuiunga mkono miradi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi amezipongeza juhudi zinazochukuliwa na Ubalozi wa India nchini Tanzania kwa kuiunga mkono Zanzibar katika kuimarisha miradi ya maendeleo ikiwamo ya majisafi na salama.

Rais Dk. Mwinyi aliyasema hayo jana katika mazungumzo kati yake na Balozi wa India, Binaya Srikanta Pradhan, Ikulu. Rais Dk. Mwinyi alisema, katika kipindi kifupi tangu balozi huyo alipoanza kazi zake Tanzania, amefuatilia kwa karibu utekelezaji wa miradi inayotekelezwa kupitia nchi hiyo hatua inayofaa kupongezwa.

Alisema ipo haja ya kuendelea kufuatilia kwa karibu miradi hiyo ili kutekelezwa kwa wakati uliopangwa ikiwamo miradi mikubwa ya majisafi na salama ambayo ujenzi wake unaendelea.

Akieleza kuhusu uendelezaji wa miradi mikubwa wa maji, Rais Dk. Mwinyi alipongeza hatua zilizofikiwa katika uendelezaji wa miradi hiyo na kueleza matumaini yake ya kukamilika kwa wakati miradi hiyo ambayo inatekelezwa kwa ushirikiano wa pamoja kati ya Benki ya Exim ya India kwa njia ya mkopo wa masharti nafuu kwa kushirikiana na Serikali ya Zanzibar.

Kwa upande wa utekelezaji wa rasilimali watu, Dk. Mwinyi aliupongeza mpango wa Serikali ya India wa kutoa nafasi za masomo kwa Tanzania ikiwamo Zanzibar na nafasi hizo za masomo zitadhaminiwa na Serikali ya India.

Aliipongeza Serikali ya India kwa nia yake ya kuanzisha chuo cha amali kisiwani Pemba na kwamba hatua hiyo itakuwa ni mchango mkubwa kwa vijana walioshindwa kuendelea na elimu ya juu Zanzibar.

Vile vile, alieleza kwamba Serikali ya Zanzibar iko tayari kutoa ushirikiano wake katika azma iliyowekwa na Serikali ya India ya kuanzisha taasisi ya teknolojia ya habari hapa nchini kwa kuwa kuwapo kwa taasisi hiyo kutasaidia kuimarisha teknolojia ya habari na mawasiliano nchini.

Naye Balozi wa India, Binaya Srikanta Pradhan, alisema India inathamini uhusiano na ushirikiano wa kihistoria uliopo kati yake na Zanzibar na atahakikisha unaisimamia vyema miradi yote inayotekelezwa na nchi hiyo.

Alieleza matarajio yake makubwa na kumhakikishia Rais Dk. Mwinyi kwamba miradi mikubwa wa majisafi na salama ambayo ujenzi wake unaendelea hivi sasa itakamilika kwa wakati uliopangwa.



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akijumuika na wananchi wa Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja, katika futari maalum aliyowaandalia juzi. Kushoto ni Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja, Idrisa Mustafa Kitwana, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Sheria, Katiba, Utumishi na Utawala Bora, Haroun Ali Suleiman (kulia), Mufti Mkuu wa Zanzibar, Shekhe Saleh Omar Kaabi (wa pili kushoto) na Naibu Katibu Mkuu wa CCM Zanzibar, Dk. Abdalla Mabodi. **PICHA: IKULU**

# Maonyesho ya biashara kupamba miaka 58 ya Muungano

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KATIKA kuadhimisha miaka 58 ya Muungano, Serikali ya Zanzibar imeandaa maonesho maalum ya biashara ambayo yatafunguliwa na Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Hamza Hassan Juma, aliyasema hayo wakati akitoa taarifa kwa vyombo vya habari katika ukumbi wa Baraza la Wawakilishi Chukwani.

Alisema maeonesho hayo yanatarajiwa kuanza Aprili 22 na kumalizika Mei 6, mwaka huu, katika viwanja vya Maisara Mjini Zanzibar na ufunguzi rasmi utafanyika Aprili 24, mwaka huu.

Alisema maonesho hayo yatajumuisha taasisi zote 29 za Muungano zilizopo Zanzibar, taasisi za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, kampuni, wafanyabiashara na wajasiriamali.

Alibainisha kwamba Aprili 20, mwaka huu kutakuwa na kongamano kubwa na mgeni rasmi anatarajiwa kuwa Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla na litazungumzia suala la Muungano na kumbukizi wa kifo cha mwasisi wa Muungano Mzee Abeid Amani Karume aliyekuwa Rais wa kwanza wa Zanzibar na Makamu wa kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Alisema kongamano hilo linataangalia mahali nchi ilipotoka, ilipo na inakoelekea, fursa na changamoto zilizopo ndani ya Muungano na kuangalia njia za kuumarisha zaidi.

"Hakuna jambo ambalo halina changamoto kwenye fursa tutasema na changamoto tutasema hivyo niwaombe wananchi wasikose kuja katika kongamano hili lina manufaa makubwa kwao na vizazi vyetu," alisema.

Hata hivyo, alisema changamoto za Muungano zimepungua ikilinganishwa na faida nyingi zilizopo ikiwamo fursa ya watu kuishi ndani ya eneo lolote la Jamhuri ya Muungano bila ya kizuizi, Wazanzibari kumiliki ardhi kubwa ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na aliwasisitiza wananchi kuona umuhimu wa Muungano wao.

Aidha, Waziri Hamza alisema katika maonesho hayo jumla ya taasisi 29 za Muungano zitashiriki ili kutoa fursa kwa wananchi kuzijua taasisi zinazowaunganisha pia kupata huduma kwa urahisi.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**KATIKA MAHAKAMA KUU TANZANIA**
**MASJALA NDOGO TEMEKE**
**(TEMEKE KITUO JUMUISHI HUDUMA ZA MAHAKAMA MIRATHI NA NDOA)**
**MIRATHI NAMBA 69 YA MWAKA 2022**
**MAOMBI YA BARUA ZA USIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU**
**MODESTUS JOSEPH MGIMWA**
**SALOME ASHERY MBANGILE......MWOMBAJI**

**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(KANUNI YA 75)**

Watuw wote wanaodai kuwa na haki ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua za usimamizi wa mirathi kwa mwombaji hapo juu

Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandiikishwa mnamo au kabla ya tarehe 06 mwezi wa 06 mwaka 2022

**Imesainiwa dar es salaam leo tarehe 13 mwezi wa 04 mwaka 2022**

NAIBU MSAJILI

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ANASTAZIA FLAVIAN MARANDU** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **SUZUKI ESCUDO** yenye namba za **USAJILI T321 AZL, CHASSIS NAMBA TD51W104478, ENGINE NAMBA J20A111119.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA: KIL/MOS/RB/210487/2020**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA DODOMA**
**MAHALI DODOMA**
**RUFAA NA.235 YA MWAKA 2021**
**BAINA YA**
**MANG'UNDA MAZOYA............MRUFANI**
**DHIDI YA**
**DANIEL MZULA ........................ MRUFANIWA**

**KWA: DANIEL MZULA**
**POPOTE ULIPO**

**YAH: KUITWA SHAURINI**

Kwa kuwa muombaji ameleta maombi yake ambayo maelezo yake yameelezwa katika Nakala ya Maombi inapatikana katika Baraza hili.

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria katika Baraza hili wewe binafsi, Wakili au Mwakilishi yeyote ambaye anaruhusiwa kisheria tarehe 02/05/2022 saa 3:00 asubuhi. Kwa mujibu wa maombi hayo unatakiwa kuleta utetezi wako kwa maandishi.

**ANGALIZO: -** kama haukuhudhuria tarehe iliyotajwa hapo juu, Baraza likidhibitisha kuwa umepokea hati ya Wito, Baraza linaweza kutoa Hukumu dhidi yako.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na Lakiri /Muhuri wa Baraza hili leo tarehe 17 ya Mwezi wa Machi,2022.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA (MAHAKAMA)**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO Enaboishu**
**WILAYA YA Arumeru**
**SHAURI YA MADAI YA 2022**
**MARCELINA JOEL KAHANGWA**
**Dhidi ya Mdai**
**VICTOR ALPHONCE....MDAIWA**

**HATI YA KUITWA SHAURINI (SUMMONS GENERAL)**
**(MCA Na.2/1984)**

Kwa Victor Alphonce wa Mwanza .

Kwa kuwa umelazimika uhudhurie mahakamani ili ujibu shtaka/ madai kuwa shahidi kama ifuatavyo .

FIKA MAHAKAMANI KUJIBU MADAI YA TALAKA ,UNAAMRIWA NA JAMHURI uhudhurie mbele ya mahakama hii siku ya J'nne tarehe 03.05.2022 saa 3:00 asubuhi au mara baada ya hapo ili shauri hili liweze kusikilizwa.

USIKOSE KUHUDHURIA

Fahamu kwamba ukikataa kupokea hati hii na kuweka sahihi yako au ukipokea na kuacha kuhudhuria mahakamani ni kosa K/f Na.114 Sura 16 K/A.

Hivyo mahakama inaweza kukuchukulia hatua kali za kisheria .

HATI HII IMETOLEWA NA AMRI YANGU NA MUHURI WA MAHAKAMA HII LEO TAREHE 13.04.2022

.....................

**HAKIMU**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA IKIKETI BUKOBA**
**LAND CASE REVISION NO. 8 OF 2020**
**(Ikitokana na Land Appeal No. 156 of 2010 katika Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya Bukoba)**
**AHAMADA SULEIMAN ...........MUOMBAJI**
**DHIDI YA**
**ZURAIKA HARUNA .................MUJIBU MAOMBI**
**ZURAIKA HARUNA C/O WEO - BAKOBA 0676987762**

**YAH: TAARIFA YA SIKU YA KUSIKILIZWA**

Kwa kuwa, mleta maombi AHAMADA SULEIMAN amewasilisha maombi yake dhidi yako, yaliyosajiliwa kama LAND CASE REVISION 08 OF 2020. Unapewa taarifa ya kwamba maombi hayo yamepangwa kusikilizwa tarehe 27/4/2022 saa 3:00 asubuhi mbele ya Mheshimiwa Jaji Ngigwana E.L.

Unatakiwa kuhudhuriwa wewe mwenyewe au kupitia kwa wakili wako. Unapewa taarifa zaidi kwamba kushindwa kuhudhuria kwako muda na tarehe iliyopangwa maombi hayo yatasikilizwa bila wewe kuwepo.

**Imetolewa kwa mkono wangu na chapa ya mahakama leo siku ya Jumatano tarehe 17/03/2022.**

.......................................

**Odira A. Amworo**
**NAIBU MSAJILI**
**MAHAKAMA KUU - BUKOBA**

## KUPOTEA KWA CHETI



ELIZABETH JOHN MAKELELE, anatangaza kupotelewa na cheti cha DIPLOMA IN NURSING AND MIDWIFERY chenye usajili namba NS4733/0019/2014 kilichotolewa na NACTE kupitia chuo cha KIBOSHO SCHOOL OF NURSING mwaka 2014. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha Polisi.

Taarifa ya Polisi: PWA/BAG/RB/44524/2022

## KUPOTEA KADI YA GARI

**SADIK ABDALLAH KILUVIA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **NISSAN CARAVAN** yenye **USAJILI NAMBA T111 CBA, CHASSIS NAMBA VWGE24805781, ENGINE NAMBA QD32209790.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA: ARU/ARU/R/154299/2022**

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA MAHAKAMA YA TANZANIA.**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya SONGEA kituo cha Mjini Mkoa wa Ruvuma .**
**Shauri la Madai Namba 17/2022.**
**Jina la Mdai BODI YA WADHAMINI YA USHIRIKA WAUZA SAMAKI SONGEA.**
**Jina la Mdaiwa SAID JAFARI ZUBERI.**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA.**

Kanuni ya 18 ya Kanuni za taratibu ,Madai katika Mahakama za Mwanzo kwa **SAID JAFARI ZUBERI.**

Kwa kuwa Mdai /Wadai ameleta /Wameleta madai yake/yao kwamba Eleza hapa habari za Madai ya TSH.26,875,079,00=Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 29 mwezi 04 mwaka 2022 saa 2:30 asubuhi /Mchana kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa Shauri hili lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.

**ANGALIZO.**

Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ukipokea hati ya kuitwa shaurini , Mahakama inaweza kusikiliza shauri hilo bila wewe kuwepo.

**Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 13 mwezi 04 mwaka 2022.**

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION**
**CAUSE NO 111 OF 2021**
**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE**
**ERASTO HUSSEIN MWINYIPEMBE .... DECEASES**
**AND**
**IN THE MATTER OF AN APPLICATIONFOR LETTERS OF ADMINISTRATION**
**ELIMRIMA CORNELLO KIMAMBO AND JOSHUA ERASTO HUSSEIN**

**GENERAL CITATION**
**(RULE 75 OF PROBATE RULES GN.369 OF 1963)**

ALL PERSON Claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Admirations made to the above named petitioner.

Objections to the grants should be filed on or before the 19 Day of April, 2022.

Dated at Dodoma this 8th day of April, 2022.

RESIDENT MAGISTRATE


Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676

Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676

OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.
MOB: +255 - 0782253676

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharasma yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KIMATAIFA



Watu wakishuhudia daraja lililosombwa na maji kutokana na mafuriko eneo la KwaZulu-Natal nchini Afrika Kusini, inakadiriwa takribani watu 400 wamefariki dunia. **PICHA: VOA**

## Ramaphosa atangaza janga la kitaifa baada ya mafuriko

**Johannesburg,** AFRIKA KUSINI

RAIS wa Afrika Kusini, Cyril Ramaphosa ametangaza janga la kitaifa nchini humo baada ya mafuriko na mvua kubwa kusababisha vifo vya watu 443 huku akitenga dola milioni saba, kwa ajili ya janga hilo.

Katika hotuba aliyoitoa jana kwenye televisheni nchini humo Ramaphosa alisema karibu watu 48 bado hawajulikani walipo.

Rais Ramaphosa alisema mafuriko mabaya yanayolikumba taifa hilo ni janga na kuonya kwamba ukarabati wa huduma za msingi utachukua muda mrefu.

Aliongeza kwamba, bado ni tatizo kufika kwenye baadhi ya maeneo yaliyoharibiwa vibaya, zikiwamo shule 16 ambazo zimeteketea kabisa.

"Hali ya janga sawa na hatua zilizowekwa kupambana na janga la Covid-19 inahitaji uwezo wa kifedha wa ziada kusaidia katika ukarabati wa vilivyoharibika."

Mvua hiyo iliyonyesha kwa saa 24 imesababisha uharibifu mkubwa wa barabara, madaraja na nyumba na kuharibu usambazaji wa chakula na mafuta na kuwaacha maelfu bila makazi.

Rais huyo alisema inakadiriwa kwamba watu 40,000 wameachwa bila makao kutokana na mafuriko hayo.

MASHAMBULIZI RUSSIA-UKRAINE:

# Ndege ya Russia yakwama kuwachukua wanadiplomasia

**Kyiv,** UKRAINE

NDEGE iliyotumwa kutoka Moscow kuwachukua wanadiplomasia wa Russia, waliofukuzwa Ugiriki na Uhispania, imelazimika kubadili mkondo kwa kilomita 15,000 kutokana na marufuku ya ndege ya Umoja wa Ulaya.

Tovuti ya kufuatilia safari za ndege ya FlightRadar24 Reports, imeripoti.

"Wakati Hispania na Ugiriki, zikitoa nafasi mara moja kwa ndege kuingia kwenye anga yao, ndege zilizunguka nchi zingine ambazo zinadumisha marufuku ya safari za ndege za Russia," tovuti hiyo ilisema.

Iliongeza kwamba umbali wa safari hiyo ulikuwa kilomita 15,163, inakaribia safari ndefu zaidi duniani kati ya Singapore na New York.

Wanajeshi wa Russia, wanapambana kuzivunja ngome za Ukraine katika eneo zima la vita Mashariki mwa Ukraine.

Rais wa Ukraine Volodymyr Zelensky, alisema mashambulizi hayo ya Donbass ni hatua ya pili iliyokuwa imesubiriwa kwa muda mrefu katika vita hivyo.

Russia, imevitaka vikosi vya Ukraine kuweka chini silaha mara moja na kutoa kauli ya mwisho mpya kwa wanajeshi wanaoulinda mji wa bandari uliozingirwa wa Mariupol kusalimu amri.

Taarifa ya Wizara ya Ulinzi Russia, ilisema wapiganaji wa Ukraine wanaopambana dhidi ya wanajeshi wa Russia katika bandari ya Mariupol kwenye Bahari ya Azov wako katika kile imeikiita 'hali ya janga'.

Waethiopia wajiandikisha kwenda vitani Ukraine

Makumi ya vijana wa Ethiopia, wamekusanyika kwenye ubalozi wa Russia mji mkuu, Addis Ababa, kufuatia uvumi wa kuajiriwa kwa wanajeshi kupigana nchini Ukraine.

Msemaji wa ubalozi huo, Maria Chernukhina, anasema hakuna utaratibu huo unaofanywa nchini Ethiopia.

Alisema watu hao walikuwa wanaonyesha mshikamano na Russia.

"Tuna wageni wengi katika ubalozi huu wanaokuja kuunga mkono Urusi. Baadhi yao wanatuambia wako tayari kusaidia kwa njia yoyote wanayoweza. Lakini sisi sio wakala wa kuajiri," Chernukhina aliongeza.

Baadhi ya vijana hao wa Ethiopia katika ubalozi huo, walionekana wakiwa na hati zao za kibinafsi.

Kijana aliyekuwa akisubiri mlangoni alisema anatafuta mshahara mzuri kama mwanajeshi au kuajiriwa katika kazi nyingine yoyote inayopatikana akisema pia anaipenda Russia.

Wengine walisema wamesikia fununu za mishahara mikubwa nchini Russia.

Ethiopia, ilikuwa miongoni mwa nchi zilizokosa kikao cha Umoja wa Mataifa (UN) cha kupigia kura azimio kuhusu uvamizi wa Russia nchini Ukraine.

Wakati huo huo, Oleksiy Goncharenko, Mbunge wa Ukraine, ameomba silaha zaidi kutoka mataifa ya Magharibi: Ikilinganishwa na jeshi la Afghanistan, ambalo lilipokea dola bilioni 80 ya vifaa, ikiwemo silaha na risasi, msaada wa mwisho wa Marekani ulikuwa dola milioni 800.

"Dunia inapaswa kutambua kwamba tunapigana na Russia, jeshi kubwa zaidi katika bara la Ulaya na nchi yenye bajeti ya silaha mara nyingi zaidi ya Ukraine, hivyo tunahitaji silaha zaidi."

### RUSSIA YAIPA MALI VIFAA VYA KIJESHI

Mali, imepokea shehena nyingine ya vifaa vya kijeshi kutoka Russia, jana, baada ya Umoja wa Ulaya (EU). kusitisha mpango wake wa mafunzo ya kijeshi na taifa hilo la Sahel.

Mkuu wa Majeshi Mali, Meja Jenerali Oumar Diarra, alipokea helikopta mbili za kivita na rada za uchunguzi, Ofisi ya Rais Mali, ilisema katika taarifa.

Ofisi ya Rais, ilisambaza video inayoonyesha vifaa hivyo vikitolewa na ndege ya mizigo ya Russia katika uwanja wa ndege wa mji mkuu Bamako.

Diarra alitaja uungaji mkono wa Russia kwa Mali kama dhihirisho la ushirikiano wenye manufaa makubwa.

Mwezi uliopita, Mali ilipokea helikopta mbili za kivita na rada zilizotengenezwa na Russia muda mfupi baada ya ripoti kuibuka kwamba Waziri wake wa Ulinzi na Mkuu wa Jeshi la Anga, walizuru Moscow 'kisiri'.

Vyombo vya habari vya serikali vilitangaza sana mapokezi hayo na kupongeza uungaji mkono wa Russia, unaokua katika operesheni za kukabiliana na waasi.

Mali, imetetea uhusiano wake na Russia, baada ya mizozo ya kimataifa kuhusu uamuzi wa kupeleka mamluki kutoka kampuni ya kijeshi yenye utata ya Wagner mwezi Desemba.

Hali hiyo, ilisababisha kuondolewa kwa vikosi vya Ufaransa vya Operesheni Barkhane na wanajeshi wa Ulaya chini ya Kikosi Kazi cha Takuba.

Wapiganaji wa Wagner na jeshi la Mali, wamehusishwa na madai ya ukiukaji mkubwa wa haki za binadamu katika operesheni za pamoja za kukabiliana na waasi katika miezi ya hivi karibuni, ripoti ambayo Mali, imekanusha.

***• Imeandaliwa na Christina Mwakangale kwa msaada wa mtandao***

# MDUNDO.COM YAWEKA REKODI WATUMIAJI MIL. 31 ROBO MWAKA

Na Mwandishi Wetu

HUDUMA inayoongoza ya muziki wa Kiafrika Mdundo.com, imetangaza kurekodi idadi mpya ya watumiaji hai milioni 31 ndani ya Afrika katika robo ya mwaka wa 2022 ikiwa inawakilisha asilimia 49 ya ongezeko kutoka mwaka uliopita.

**Hatua hiyo inaelezwa kudhihirisha ukuaji wa huduma hii katika bara zima la Afrika ndani ya mwaka uliopita.**

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Nairobi, Kenya, Mkuu wa Brand na Partnerships kutoka Mdundo, Rachel Karanu, amesema kampuni hiyo inatambua ukuaji huo kutokana na ongezeko la uhitaji wa matumizi rahisi ya huduma za muziki wa kimtandao katika jamii hususan vijana.

Pia, amesema kampuni hiyo imeweka mikakati na washirika ambao ni makampuni makubwa ya mtandao wa simu katika bara la Afrika yanayozidi kuikuza huduma hiyo.

Alisema katika robo ya mwaka huu kampuni pia imeongeza matangazo na washirika wake tofauti tofauti jambo ambalo limechochea ukuaji huu na kuipa mdundo alama chanya zaidi huku akiwataja washirika hao kuwa ni pamoja na Benki ya Standard Chartered, East Africa Breweries Ltd, Nation Media Group, Airtel, Zenith Bank pamoja na 10Bet Africa.

"Tunaendelea kushuhudia ongezeko kubwa la uhitaji rahisi wa huduma ya muziki haswa kutoka kwa vijana ambao ndio wanatengeneza soko kubwa la wasikilizaji wa muziki ndani ya Afrika. Hitaji hili ndilo limesababisha ukuaji huu. Tutaendelea kujiimarisha kiteknolojia, katika uvumbuzi na njia mpya za kuongea na kuwashirikisha wasikilizaji wetu.

"Mkakati wetu wa kushirikisha makampuni makubwa ya mawasiliano Afrika kama MTN, Vodacom na Airtel, unaendelea kutufanya sisi kutoa jukwaa la kuwafikia wateja wetu walengwa huku tukiwapatia huduma maalum iliyotengenezwa kwa ajili yao," alisema Rachel.

Nigeria na Afrika Kusini zinaongoza kwa kuandikisha wasikilizaji zaidi katika kila robo ya mwaka, ambapo Nigeria imerekodi wasikilizaji milioni 8.3 sawa na asilimia 92 na Afrika Kusini milioni 2.2 sawa na asilimia 80.

Wasikilizaji wa Kenya wameongezeka kwa asilimia 46 kufikia watumiaji milioni 5.7 huku Tanzania ikikua kwa asilimia 10 na kufikia wasikilizaji milioni 3.8. Kumekua pia na maongezeko ya watumiaji ya maana katika nchi za Kusini mwa Sudan, Burundi, Congo, Cameroon pamoja na Ivory Coast.

Ukiacha sababu kuu ya kutoa na kuwasilisha muziki bora na unaoongoza duniani, Mdundo pia huwapatia wasikilizaji wake mchanganyiko wa ladha za ma DJ tofauti ambazo zinaweza kupakuliwa bila kulipia. Sasa hivi, Mdundo inafanya mashindano tofauti ya ma DJ kutoka nchi za Tanzania na Nigeria.

"Tuna matajario mazuri na robo ya mwaka inayofuata huku tukiendelea katika mpango wa kufikia wasikilizaji wetu walengwa katika mwaka wetu wa fedha unaoishia Juni 2022. Tutaendeleza ukuaji wetu kupitia uvumbuzi wa kiteknolojia katika kuandikisha watumiaji wapya, pamoja na kutoa jukwaa maridhawa la matangazo kwa washirika wetu," alisisitiza Rachel.



Mkuu wa Brand na Partnerships Tanzania, Abella Mutalemwa (kushoto), akikabidhi zawadi kwa Abdul Msuri ambaye ni Digital Media Manager kutoka Dentsu kwa kuendesha kampeni bora katika robo ya mwaka wa Mdundo 2022. **MPIGAPICHA WETU**

# Kidunda kutorudia makosa kwa Katompa

Na Saada Akida

BONDIA wa ngumi za kulipwa nchini, Selemani Kidunda, amesema hatorudia tena makosa yaliyopita katika mchezo wake wa marudiano dhidi ya Tshimanga Katompa kutoka DR Congo.

Kidunda anatarajia kushuka ulingoni Julai mwaka huu katika pambano la marudiano ya kuwania mkanda wa ubingwa wa WBF, litakalofanyika mjini Songea.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kidunda alisema katika pambano la awali Desemba 26, mwaka jana, ilitokea tatizo na yeye kuchanika sehemu ya jicho hali iliyosababisha mwamuzi wa pambano hilo kulivunja kutokana na kanuni za mchezo huo.

Alisema safari hii wanafanya maandalizi mazuri na kutompa nafasi mpinzani wake kurudia yaliyotokea katika pambano lililopita kwa kumpasua sehemu ya jicho.

"Kwa sasa nafanya maandalizi mazuri kuhakikisha ninafanya vizuri katika pambano hilo la marudiano, nina imani sitarudia makosa ya awali kwa sababu najiandaa kutokana na ubora wa mpinzani wangu," alisema Kidunda.

Alisema anafanyia kazi madhaifu yake baada ya kugundua pambano la kwanza alipasuka kutokana na mapungufu aliyokuwa nayo ulingoni.

Naye mwandaaji wa pambano hilo, Selemani Semunyu, alisema maandalizi ya pambano hilo yatafanyika baada ya kumalizika kwa mfungo wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhan.

Alisema kutakuwa na mabondia watakaocheza mapambano ya utangulizi kati ya Kidunda na Katompa, ambao watapatikana kwenye pambano litakalofanyika Sikukuu ya Iddi Mosi wilayani Tunduru mkoa wa Ruvuma.

"Kila kitu kinaenda vizuri na Sikukuu ya Iddi Mosi, tumeandaa pambano la kutafuta mabondia ambao watapanda ulingoni kabla ya Kidunda na Katompa kupambana," alisema Semunyu.

## Kipa Coastal Union nje wiki tatu

Na Saada Akida

KIPA namba moja wa Coastal Union, Mussa Mbissa, atakuwa nje ya uwanja kwa wiki tatu baada ya kupata majeraha ya bega la mkono wa kushoto katika mchezo dhidi ya Tanzania Prisons, imeelezwa.

Mbissa juzi alikimbizwa Hospitali Teule ya Mbeya baada ya kugongana na mchezaji wa Tanzania Prisons katika mchezo wa Ligi Kuu Bara uliopigwa juzi mkoani humo kwenye Uwanja wa Sokoine na Coastal Union kukubali kupoteza kutokana na kichapo cha bao 1-0.

Kwa mujibu wa daktari wa timu hiyo, Francis Mganga, kipa huyo aliteguka sehemu ya mbele ya bega la mkono wa kushoto na atakuwa nje wiki tatu.

"Anaendelea vizuri, tatizo si kubwa sana kama tulivyofiria baada ya kuumi, lakini amepatiwa vipimo na kugundulika tatizo, hivyo atakuwa nje ya uwanja kwa wiki tatu kwa ajili ya matitabu," alisema Mganga.

## Baraza afurahia taa Uwanja Kaitaba

Na Adam Fungamwango

KOCHA Mkuu wa Kagera Sugar, Francis Baraza, ameonyesha furaha yake kutokana na kufungwa taa kwenye Uwanja wa Kaitaba, Bukoba mkoani Kagera na kuanza kutumika kwenye mechi ya Ligi Kuu usiku kati ya timu hiyo na KMC, akidai kuwa itamaliza au kupunguza mechi nyingi za mchana wa jua kali na jioni ambazo zinawanyong'onyesha na kuwaumiza wachezaji.

Hata hivyo, Kocha Mkuu wa KMC, Thierry Hitimana, pamoja na kupongeza, alitaka mwanga kuongezwe, kwani kuna sehemu bado zinaonekana hazina mwanga wa kutosha.

Jumapili iliyopita, kwa mara ya kwanza kwenye historia ya soka Uwanja wa Kaitaba ulichezewa mechi usiku majira ya saa tatu, ukiwa umefungwa taa ambapo ni mkakati maalum wa Shirikisho la Soka nchini (TFF) na mmoja wa wadhamini wa Ligi Kuu, Azam Media Limeted, kuhakikisha baadhi ya viwanja vinakuwa na taa zitakazoweza kuchezewa soka usiku.

## ZISIKUPITE

### HAALAND SAFI CITY
KLABU ya Manchester City imefikia makubaliano binafsi na mshambuliaji wa Borussia Dortmund na Norway, Erling Haaland mwenye umri wa miaka 21. (***Mail***)

### CAVANI ATAKIWA MADRID
IWAPO mpango wa Erling Haaland hautatimia, Real Madrid wanaweza kumlenga mshambuliaji wa Manchester United na Uruguay, Edinson Cavani mwenye umri wa miaka 35 kama mbadala wake. (***Fichajes***)

### JAMES KUNG'OLEWA CHELSEA
REAL Madrid wanamfuatilia kwa karibu winga wa Chelsea, Reece James mwenye umri wa miaka 22. (***Mirror***)

### POPE KUTUA WEST HAM
KLABU ya West Ham United inatafakari uwezekano wa kumsajili golikipa wa England na Burnley, Nick Pope mwenye umri wa miaka 29. (***Times***)

### HAG MAMBO SAFI UNITED
KLABU ya Manchester United na Erik ten Hag wanakaribia kukamilisha mazungumzo yao, lakini watasubiri kutangaza rasmi mpango huo hadi kipengele cha fidia cha euro milioni mbili kwa kocha huyo wa Uholanzi kitakapomalizika. (***Fabrizio Romano***)

### RUDIGER KUTUA MADRID
REAL Madrid wanafikiria uwezekano wa kumsajili beki wa Chelsea, Antonio Rudiger mwenye umri wa miaka 29, kwa uhamisho wa bure wakati mkataba wake utakapokamilika. (***ESPN***)

### LACAZETTE, LYON WATETA
KLABU ya Lyon ni miongoni mwa klabu ambazo mshambuliaji wa Arsenal, Alexandre Lacazette mwenye umri wa miaka 30, anajadiliana nazo atakapokuwa mchezaji huru msimu ujao. (***Canal Plus***)

### POGBA KURUDI JUVENTUS
JUVENTUS wanataka kumrudisha Paul Pogba mwenye umri wa miaka 29 mjini Turin kwa uhamisho wa bure wakati mkataba wake na Manchester United utakapokamilika msimu wa majira ya joto. (***Football Italia, via Sport Mediaset***)

### GNABRY KUFUNGWA BAYERN
MLENGWA wa Liverpool, Serge Gnabry mwenye umri wa miaka 26, anafanya mazungumzo na Bayern Munich kuhusu kuongezwa mkataba. (***Goal***)

### LOWRY KUSAJILIWA NEWCASTLE
KLABU ya Newcastle ipo katika nafasi nzuri kumsajili kiungo wa kati wa Rangers mwenye umri wa miaka 18, Alex Lowry. (***Football Insider***)

### REAL MADRID WASITA
REAL Madrid wanasita kutimiza matakwa ya mshahara wa Erling Haaland kwa sababu hawataki kujivuruga kwa kumfanya mshambuliaji huyo kuwa mchezaji anayelipwa fedha nyingi zaidi kikosini. (***Goal***)

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# HAZARD HATAONDOKA TENA MADRID, KUONYESHA UBORA

Kama Rais Florentino Perez atamtaka aondoke, basi hatoweza kucheza hapo, lakini nawahakikishia kwamba...

**MADRID,** HISPANIA

MDOGO wa nyota wa Real Madrid, Eden Hazard, Kylian amesema kwamba mchezaji huyo hana mpango wowote wa kutaka kuondoka klabuni hapo akisisitiza kwamba anataka kujidhihirisha yeye mwenyewe.

Hatima ya Hazard pale Bernabeu ipo katika mjadala na huenda klabu hiyo ikaamua kumuuza wakati wa dirisha la majira ya joto na taarifa za hivi majuzi zilidai Arsenal wapo tayari kumnasa mchezaji huyo.

**"Eden Hazard hatoondoka Madrid hadi atakapojionyesha kwamba yupo imara," alisema Kylian akiiambia RTL.**

"Ameonyesha kwenye klabu ambayo anaichezea na kwa maoni yangu hana mpango wa kuondoka. Siamini kama ataondoka."

"Kama Rais Florentino Perez atamtaka aondoke, basi hatoweza kucheza hapo sidhani kama ataendelea kubaki.

"Lakini naweza kuwahakikishia kwamba atafanya kila linalowezekana kuonyesha kwamba yeye ni mchezaji bora wa Real Madrid."

LIVE IN PLAY
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 1,171,

MECHI KALI
CHELSEA
VERSUS
ARSENAL
1 | 1.83
X | 3.48
2 | 4.07

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# BARCELONA WAREJEA TENA KWA MARTINEZ

**BARCELONA,** Hispania

BARCELONA wameripotiwa kuwa wamerejesha nia yao ya kutaka kumnunua mshambuliaji wa Inter Milan, Lautaro Martinez.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24, amekuwa katika kiwango kizuri na kufanikiwa kupachika mabao katika klabu yake ya Italia wakati wa kampeni ya msimu huu wa 2021-22, akifunga mabao 17 kwenye mechi 41 za mashindano yote.

Martinez bado ana zaidi ya miaka minne kabla ya kumaliza mkataba wake wa sasa, lakini kumekuwa na uvumi mwingi kuhusu mustakabali wake katika miezi ya hivi karibuni, huku klabu kadhaa zikiwamo Arsenal, Atletico Madrid na Tottenham Hotspur zikihusishwa na kuitaka huduma yake. Barcelona ilitarajiwa sana kumsajili mchezaji huyo wa kimataifa wa Argentina katika msimu wa majira ya joto wa 2020, lakini mlipuko wa COVID-19 ulifanya isiwezekane kwa uhamisho huo kukamilika.

Kwa mujibu wa Sport, klabu hiyo ya Katalunya sasa imefufua nia yao, ikimtazama mshambuliaji huyo kama chaguo la bei nafuu dhidi ya Erling Haaland wa Borussia Dortmund na Robert Lewandowski wa Bayern Munich.

Ripoti hiyo inadai kuwa Inter wana nia ya kumsajili Memphis Depay kutoka kwa timu ya Xavi, hivyo mchezaji huyo wa kimataifa wa Uholanzi anaweza kutumika kuongeza nguvu.



# Ronaldo afiwa na mtoto wa kiume

**MANCHESTER,** England

NYOTA wa Manchester United, Cristiano Ronaldo na mpenzi wake, Georgina Rodriguez wametangaza kifo cha mtoto wao wa kiume, wakisema kwamba ni uchungu mkubwa mbao mzazi yeyote anaweza kuhisi.

Raia huyo wa Ureno mwenye umri wa miaka 37, na Rodriguez (28), walikuwa wakitarajia kupata mapacha.

Mtoto wao wa kike alinusurika na wamesema kuzaliwa kwake kuliwapatia nguvu ya kuishi muda huu wakiwa na matumaini na furaha.

"Mtoto wetu wa kiume wewe ni malaika wetu. Tutakupenda maisha yetu yote," waliandika kupitia Instagram.

"Ni huzuni kubwa kwam tunatangaza kifo cha mtoto w kiume aliyefariki. Tumegha habishwa na kifo hiki na sasa naomba kuwa na faragha wak huu mgumu."

Wawili hao walitangaza kupa ujauzito huo Oktoba mwaka ul pita.

Timu ya Man United ilichapis ujumbe katika mtandao wao w twitter ikisema: "Uchungu wa ni uchungu wetu."

Timu ya zamani ya Ronald Real Madrid, rais wake pamo na bodi ya wakurugenzi waliser "wamehuzunishwa sana" na l ongeza: "Real inahisi maumivu wazazi hao na inawatakia sub na nguvu wakati huu".

**HABARI MICHEZO**

# ,243,460

# JACKPOT
## MECHI WIKI HII

**BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13**

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 23/04/22 | 17:00 | Leicester vs Aston Villa | 2.63 | 3.28 | 2.53 |
| 02. 23/04/22 | 17:00 | Hull City vs Reading | 2.48 | 3.17 | 2.77 |
| 03. 23/04/22 | 17:00 | Birmingham vs Millwall | 2.78 | 3.08 | 2.53 |
| 04. 23/04/22 | 17:15 | Fuenlabrada vs Ponferradina | 2.57 | 3.16 | 2.67 |
| 05. 23/04/22 | 20:30 | Adana Demirspor vs Trabzonspor | 2.40 | 3.39 | 2.74 |
| 06. 23/04/22 | 21:00 | Waalwick vs PEC Zwolle | 2.46 | 3.07 | 2.87 |
| 07. 23/04/22 | 21:30 | St. Pauli vs SV Darmstadt | 2.52 | 3.31 | 2.62 |
| 08. 24/04/22 | 16:00 | Burnley vs Wolverhampton | 2.69 | 2.98 | 2.69 |
| 09. 24/04/22 | 16:00 | Bologna vs Udinese | 2.87 | 3.17 | 2.41 |
| 10. 24/04/22 | 16:00 | Metz vs Brest | 2.98 | 3.22 | 2.33 |
| 11. 24/04/22 | 17:15 | UD Ibiza Eivissa vs Las Palmas UD | 2.79 | 3.13 | 2.49 |
| 12. 24/04/22 | 18:30 | Hertha BSC vs Stuttgart | 2.73 | 3.22 | 2.48 |
| 13. 24/04/22 | 21:45 | Lazio vs AC Milan | 2.78 | 3.27 | 2.41 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

## JUMATANO - 20/04/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 16:00 | 2127 | Zesco United vs Lusaka Dynamos | 1.89 | 3.02 | 4.19 |
| 16:00 | 3558 | Chambishi FC vs Zanaco | 3.37 | 2.54 | 2.44 |
| 16:00 | 5431 | Nkana FC vs Buildcon | 2.24 | 2.78 | 3.41 |
| 19:00 | 2418 | MFK Karvina vs Pardubice | 2.10 | 3.38 | 3.48 |
| 19:00 | 2995 | Bohemians vs Hradec Kralove | 2.43 | 3.14 | 3.04 |
| 19:00 | 3165 | Slovacko vs Slovan Liberec | 1.87 | 3.64 | 3.99 |
| 19:00 | 3382 | Lech Poznan vs Gornik Leczna | 1.12 | 6.82 | 16.55 |
| 19:00 | 4063 | Sigma Olomouc vs Sparta Prague | 4.04 | 3.69 | 1.85 |
| 19:00 | 4426 | Banik Ostrava vs Baumit Jablonec | 2.07 | 3.49 | 3.44 |
| 19:00 | 4976 | Mlada Boleslav vs Viktoria Plzen | 3.37 | 3.47 | 2.10 |
| 19:00 | 5474 | Slavia Prague vs Zlin | 1.14 | 7.89 | 17.19 |
| 19:00 | 5632 | Teplice vs Ceske Budejovice | 2.12 | 3.47 | 3.32 |
| 19:30 | 3082 | CSKA Moscow vs Spartak Moscow | 2.11 | 3.26 | 3.12 |
| 19:45 | 2679 | Udinese vs Salernitana | 1.48 | 4.26 | 5.95 |
| 20:00 | 1741 | Mjallby vs Sirius FK | 1.88 | 3.26 | 3.84 |
| 20:00 | 1866 | Atletico Madrid vs Granada | 1.30 | 5.19 | 9.38 |
| 20:00 | 2000 | Troyes vs Clermont Foot | 2.28 | 3.20 | 3.10 |
| 20:00 | 2448 | Lorient vs Metz | 1.76 | 3.53 | 4.47 |
| 20:00 | 3042 | NewellS Old Boys vs Banfield | 2.43 | 2.93 | 2.88 |
| 20:00 | 3959 | Monaco vs Nice | 1.82 | 3.63 | 3.98 |
| 20:00 | 4002 | Hajduk Split vs Dinamo Zagreb | 2.58 | 3.16 | 2.53 |
| 20:00 | 4503 | AIK Football vs Varbergs Bois | 1.54 | 3.74 | 5.43 |
| 20:00 | 4568 | Norrkoping vs BK Hacken | 2.22 | 3.40 | 2.82 |
| 20:00 | 4647 | Bordeaux vs St Etienne | 2.40 | 3.28 | 2.83 |
| 20:00 | 4781 | Reims vs Lille | 3.43 | 3.13 | 2.16 |
| 20:00 | 4915 | GIF Sundsvall vs Kalmar | 4.09 | 3.55 | 1.74 |
| 20:00 | 5217 | IFK Goteborg vs Djurgardens IF | 2.63 | 3.16 | 2.48 |
| 20:30 | 2733 | Independiente DV vs Deportivo Cuenca | 1.38 | 4.28 | 7.01 |
| 20:30 | 3513 | Alanyaspor vs Sivasspor | 2.23 | 3.35 | 3.10 |
| 21:00 | 2463 | FC Gyori Eto vs Ferencvaros TC | 13.61 | 6.80 | 1.14 |
| 21:00 | 2984 | Celta Vigo vs Getafe | 2.17 | 3.01 | 3.61 |
| 21:30 | 1892 | Pogon Szczecin vs Rakow Czestochowa | 2.25 | 2.98 | 3.12 |
| 21:45 | 1605 | Newcastle vs Crystal Palace | 2.28 | 3.17 | 3.07 |
| 21:45 | 1707 | Everton vs Leicester | 2.25 | 3.33 | 2.98 |
| 21:45 | 2551 | Chelsea vs Arsenal | 1.83 | 3.48 | 4.07 |
| 21:45 | 5896 | RB Leipzig vs Union Berlin | 1.47 | 4.45 | 6.48 |
| 22:00 | 1408 | Brest vs Lyon | 4.18 | 3.93 | 1.72 |
| 22:00 | 1518 | Manchester City vs Brighton | 1.22 | 5.64 | 12.34 |
| 22:00 | 4650 | Marseille vs Nantes | 1.63 | 3.84 | 4.99 |
| 22:00 | 4654 | Angers vs Paris St Germain | 6.67 | 4.63 | 1.41 |
| 22:00 | 5091 | Juventus vs Fiorentina | 1.94 | 3.33 | 3.85 |
| 22:00 | 5108 | Lens vs Montpellier | 1.73 | 3.78 | 4.28 |
| 22:00 | 5536 | Strasbourg vs Rennes | 2.54 | 3.29 | 2.64 |
| 22:15 | 5099 | Mafra vs Tondela | 2.20 | 3.25 | 2.96 |
| 22:30 | 1117 | El Gouna vs Smouha Club | 3.08 | 2.94 | 2.44 |
| 22:30 | 2811 | Patronato Parana vs Racing Club | 3.40 | 3.11 | 2.07 |
| 22:30 | 4621 | Velez Sarsfield vs Central Cordoba | 1.94 | 3.11 | 3.79 |
| 22:30 | 5616 | Osasuna vs Real Madrid | 4.58 | 3.68 | 1.72 |
| 23:00 | 1880 | AD Grecia vs AD Guanacasteca | 1.81 | 3.31 | 4.08 |
| 23:00 | 4587 | Orense SC vs LDU Quito | 3.12 | 3.12 | 2.18 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# SIMBA YAANZA KUIANDALIA MKAKATI ORLANDO PIRATES

**Saada Akida na Dennis Fussi**

KUELEKEA mechi ya marudiano ya robo fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Orlando Pirates ya Afrika Kusini, Simba imesema wataenda kucheza kwa tahadhari na kuwaheshimu wapinzani wao, lengo likiwa ni moja tu kufuzu hatua ya nusu fainali.

**Simba ambayo imeingia kambini jana tayari kwa maandalizi ya mechi hiyo ya marudiano itakayopigwa Jumapili wiki hii nchini Afrika Kusini, inahitaji sare yoyote ama ushindi wowote ili kutinga nusu fainali kutokana na mechi ya awali katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam kushinda bao 1-0.**




Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Simba, Pablo Franco, alisema anaimani kubwa na timu hiyo kucheza nusu fainali hasa kama wachezaji wakijitoa na kuwa makini katika mchezo huo wa marudiano.

Alisema ni mechi ngumu na ya ushindani mkubwa kwa sababu wanahitaji kujilinda, lakini pia ikiwezekana kutafuta bao la mapema ilhali Orlando Pirates nao wakihitaji kutafuta ushindi zaidi ya bao 1-0.

"Matokeo tuliyoyapata nyumbani ni faida kubwa kwetu katika mchezo wa marudiano, tunatakiwa kwenda kwa kuwaheshimu wapinzani wetu na kucheza kwa tahadhari kubwa ili kufikia malengo yetu ya kucheza nusu fainali," alisema Pablo.

Naye nahodha Msaidizi wa Simba, Mohammed Hussein 'Zimbwe Jr', alisema ushindi walioupata nyumbani hautawafanya kubweteka na kwamba watahakikisha wanaenda kucheza kwa nidhamu ya hali ya juu.

Alisema Orlando walicheza kwa kuwaheshimu na kutumia muda mwingi kujilinda ili kuhakikisha hawafungwi mabao mengi kitu ambacho wanatakiwa kwenda kufanya wao wanapokwenda kucheza mchezo huo wa marudiano.

"Tunajua Orlando wakiwa kwao hawatacheza kama walivyocheza hapa, walituheshimu nasi tunaenda kwao tutawaheshimu kwa kucheza kwa nidhamu ya hali juu ili kutimiza ndoto ya kila mchezaji kuona timu ikiingia nusu fainali," alisema.

Kwa upande wa Meneja Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, alisema wanajua umuhimu wa mchezo huo, hivyo wamejipanga na hawatarudia makosa waliyofanya msimu uliopita kwa kufungwa na Kaizer Chiefs na kutolewa hatua ya robo fainali Ligi ya Mabingwa Afrika.

"Tunajua wapo mashabiki walitamani tushinde mabao matatu, manne au matano, ila niwakukumbushe hii ni robo fainali, wanaofungwa idadi kubwa ya mabao wanaishia hatua ya makundi.

"Tumemalizana na Orlando hapa nyumbani, sasa akili zetu na nguvu tunaelekeza mechi ya marudiano kwao Soweto. Tupo tayari kwa mabapambano na safari hii hatutarudia makosa," amesema Ally.

# *Namungo yaiengua Azam, yaigeukia Yanga*

**Adam Fungamwango na Shufaa Lyimo**

USHINDI wa mabao 3-1 ilioupata dhidi ya Ruvu Shooting, unaifanya timu ya Namungo kuiengua Azam FC kwenye nafasi ya tatu ya msimamo wa Ligi Kuu, huku Kocha Msaidizi wa timu hiyo, Jamhuri Kihwelo 'Julio' akidai lengo lao bado ni kutwaa ubingwa na kwa watapambana hadi dakika ya mwisho, hesabu zitakapogoma.

Akizungumza baada ya mechi hiyo kwenye Uwanja wa Ilulu mjini Lindi, Julio alisema kuwa wachezaji wao walipambana kadri ya uwezo wao na kuweza kupata ushindi ambao umekuwa muhimu kwenye klabu hiyo ambayo ina malengo ya kucheza mechi za kimataifa msimu ujao.

"Mpaka sasa hatujakata tamaa za kuusaka ubingwa, lengo letu ni ubingwa mpaka hapo mahesabu yatakapokataa, na umeona David Molinga amefunga bao, unajua hivi sasa ligi inaelekea mwishoni, kila mchezaji anapambana ili kujiwekea mazingira mazuri kuweza kusajiliwa msimu ujao," alisema Julio.

Kwa ushindi huo, Namungo imekwea hadi nafasi ya tatu, ikifikisha pointi 29 kwa mechi 20 ilizocheza, ikiacha Azam ikiporomoka hadi nafasi ya nne ikiwa na pointi 28, ikicheza mechi 19.

Aidha, Julio alisema baada ya kuzoa pointi hizo tatu kutoka kwa Ruvu Shooting, sasa wanaelekeza nguvu zao kwenye mchezo ujao dhidi Yanga, April 23, mwaka huu.

"Baada ya kumfunga Ruvu sasa akili na nguvu zetu tunazielekeza kwenye mchezo wetu ujao dhidi ya Yanga. "Tutapambana kuhakikisha hatupotezi mchezo huo tunaomba mashabiki wetu waendelee kutuunga mkono," alisema.

Naye Kocha Mkuu wa Ruvu Shooting, Charles Boniface Mkwasa amesema wachezaji wake walikuwa wakipoteza mipira mingi wanapoingia ndani ya eneo la hatari la wapinzani wao, hivyo mpira unaporudi kwao wanaadhibiwa.

# Michezo

Jumatano Aprili 20, 2022

Nipashe




Ronaldo afiwa na mtoto wa kiume UKURASA 22

# Simba yamzulia balaa kocha Orlando Pirates

## ●●● Sasa akalia kuti kavu, mashabiki wacharuka wataka benchi zima la ufundi lifutwe kazi, wasema hata kama...

**Na Mwandishi Wetu**

LICHA ya dakika 90 za pili za mechi ya marudiano ya robo fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika zikisubiriwa kuamua timu itakayotinga nusu fainali kati ya Orlando Pirates na Simba, Jumapili wiki hii, mashabiki wa miamba hiyo ya Afrika Kusini wamecharuka wakitaka Kocha wa 'Buccaneers' hao, Mandla Ncikazi na mwenzake, Fadlu Davids, kutimuliwa.

**Hatua hiyo, imekuja baada ya Orlando Pirates kukubali kipigo cha bao 1-0 dhidi ya Simba katika mechi ya robo fainali ya kwanza iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam Jumapili iliyopita, shukrani kwa Shomari Kapombe aliyefunga bao hilo pekee kwa mkwaju wa penalti dakika ya 67 baada Bernard Morrison kuchezewa madhambi ndani ya eneo la hatari.**

Pamoja na Ncikazi kushusha lawama kwa mwamuzi wa mechi hiyo kuwa aliibeba Simba pamoja na shutuma nyingi kwa waamuzi waliokuwa chumba cha VAR, kwamba walizima mtambo kwa lengo la kuwabeba wenyeji, lakini mashabiki wa timu hiyo wametaka atimuliwe na msaidizi wake kutokana na uwezo wao mdogo kiufundi.

Mashabiki wa Orlando Pirates wameutumia mtandao wa kijamii wa klabu hiyo kuelezea mfadhaiko wao kutokana na matokeo hayo wakitaka Ncikazi na kocha mwenzake, Davids kutimuliwa.

Hizi hapa ni baadhi ya ujumbe kati ya nyingi zilizotumwa katika mtandao wa klabu hiyo baada tu ya matokeo hayo ya Jumapili:-

Tusipoamka na habari kwa ufupi kesho, nitapumzika kushabikia hii Mandla Ncikazi FC, nimechoka kudhalilishwa hivi. ***#NcikaziLazima Aondoke (@NkarnyiK_88)***

Orlando Pirates imekufa. Njia pekee ya kuirejesha ni kuwafukuza wote wawili Mandla na Fadlu. Achia Ndlovu, Mphontshane, Mabaso, Mntambo, Djvukamanje, Dlamini, Pepra, Lepasa na ununue wachezaji wenye ubora. – huwi***_freeman (@NMochelete) Aprili 17, 2022***

Angalau tumebakiza mechi tano au zaidi kabla ya mwisho wa msimu. Nimemchoka huyu jamaa. Tangu amefika hakuna mabadiliko kabisa ya kuonyesha kuwa kuna mtu mpya mwenye mamlaka!!!– ***Mogomotsi Mhure (@TheRealPanyasa) Aprili 17, 2022***

@orlandopirates ni wakati wake wa kuwaruhusu wawili hao wa muda kurudi kwenye timu zao ndogo, wamepoteza muda na nafasi zetu vya kutosha. – ***Lindisipho_Psyfo (@Sipho_Psyfo5) Aprili 17, 2022***

Hatuheshimiwi kama mashabiki wa Orlando Pirates. Ncikazi na Fadlu ni makocha wa daraja la kawaida, lazima waende. Irvin Khoza lazima pia aamue kama bado anataka kuinoa timu hii au la, huu ni upuuzi.– ***NativeOfGiyani (@Tlangelani87) Aprili 17, 2022***

Inaonekana kama timu hii ya ufundi ya Orlando Pirates ina mizozo mingi sana na wachezaji wakubwa, ambao hawafai vya kutosha kwa klabu kubwa.– ***Boksbrizio (@Boks_26) Aprili i17, 2022***

Orlando Pirates inacheza aibu ya takataka. – ***Dumizulu Ka Nkwanyana (@LaDumezulu) April 17, 2022***

#Ncikazi Lazima Aondoke Orlando Pirates wanacheza soka la kutatanisha sana chini ya makocha hawa wawili wa kawaida wasio na uzoefu wa timu kubwa, wanachezesha wachezaji wa kawaida kama Dlamini, Ndlovu, Peprah huku tuna wachezaji kama Mhango, Lorch, Mntambo, Lepasa@orlandopirates #Pirates. – ***Khayelihle (@Khaye_Mabaso) Aprili 17, 2022***

Makocha hawa lazima waondoke ili kumaliza kutuletea sifa mbaya@orlandopirate.– Engineer Matšhela Koko, MBL ***(@koko_matshela) Aprili 17, 2022***

Mpira wa Ncikazi ndio mbaya zaidi. Soka la kutisha nililolishuhudia. 'Subs' (watokea benchi) walikuwa wabaya zaidi. @orlandopirates– ***KING XERXES (@MorganBilal) Aprili 17, 2022***

Wakati huo huo baadhi ya mashabiki walikataa kumlaumu Ncikazi badala yake wamemuunga mkono kwa kitendo chake cha kukerwa na matumizi ya VAR na kauli yake ya madai kuwa mwamuzi aliisaidia Simba nchini Tanzania.

@CAF_Mtandaoni . VAR haina maana barani Afrika. Timu zinaibiwa mbele ya VAR. Mchezo kati ya Al Ahly dhidi ya Raja Casablanca; Simba Vs Orlando Pirates. Waamuzi hao hawakukuwahi kurekebishwa na VAR licha ya kufanya makosa makubwa– ***Mashudu Chairman Mundalamo (@Shudulizah2) Aprili 17, 2022***

@orlandopirates wamecheza Africa kwa miongo kadhaa, matukio ya nje ya uwanja yanatarajiwa, lakini wakati kuna VAR ungetegemea uwanjani majambazi yatashughulikiwa lakini maafisa walithibitisha kuwa VAR hii itumike tu kuendeleza nia zao na sio kurekebisha. makosa yao https://t.co/WJpT1aWWaf– ***Konke Ndaba (@ndabasbonga) Aprili 17, 2022.***



Khalid Aucho akiwa mazoezini tayari kwa mechi ijayo dhidi ya Namungo FC. **PICHA: YANGA**

# Hersi afunguka ya Aucho

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Yanga imewataka wanachama na mashabiki wake kupuuza taarifa kuwa mchezaji wao, Khalid Aucho anaidai klabu hiyo na amesusa, hivyo kutoonekana kwa muda sasa akiitumikia uwanjani.

Mkurugenzi wa Uwekezaji wa GSM ndani ya klabu hiyo , Injinia Hersi Said, amesema hizo ni propaganda za kitoto alizoziita pia ni za maji taka ambazo nia yake ni kutaka kuwaondoa kwenye azma yao ya kutaka kutwaa ubingwa msimu huu.

"Aucho alikuwa majeruhi na niseme tu tayari ameshaanza mazoezi, siku chache zijazo ataonekana uwanjani. Nieleze wazi tu kuwa yeye ni mchezaji anayependa kucheza mpira, tuna mkataba naye wa miaka miwili na ndiyo kwanza ameutumikia mmoja, haidai klabu hata shilingi moja, anaipenda klabu na anajitolea kwa ajili ya timu," alisema Hersi ambaye pia ni Mjumbe wa Kamati ya Usajili wa klabu hiyo.

Alisema kuwa hizo ni propaganda zinazoenezwa na watu wenye nia ovu dhidi ya klabu hiyo, wakidhani kuwa wataidhohofisha kwenye njia yake ya kutaka kutwaa ubingwa.

"Hizi ni propaganda za kitoto na za maji taka, Yanga tumeshavuka huko, haya mambo yanatengenezwa sijui kwa manufaa ya nani, lakini niseme tu hayana afya, niwatoe tu hofu wanachama na mashabiki wa Yanga, si Aucho tu, hakuna mchezaji yoyote anayeidai klabu, hayo yalikuwa ni miaka mitatu iliyopita. Kwa sasa tuna mkataba na wadhamini wetu ambao wanawalipa kwa wakati," alisema.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >